



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

**TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2017,
HADI JANUARI, 2018**

[*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*]

Ofisi ya Bunge,
S.L.P. 941,
DODOMA

FEBRUARI, 2018

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA.....	1
1.0 MAELEZO YA JUMLA	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Majukumu ya Kamati	4
1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati.....	5
1.4 Shughuli zilizofanyika.....	6
SEHEMU YA PILI.....	11
2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI	11
2.1 Maelezo ya Jumla	11
2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati	12
2.3 Matokeo ya Semina zilizofanyika.....	35
SEHEMU YA TATU.....	37
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO	37
3.1 Maoni	37
3.2 Mapendekezo.....	40
SEHEMU YA NNE	46
4.0 HITIMISHO	46
4.1 Shukurani	46
4.2 Hoja	47

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO
YA NJE, ULINZI NA USALAMA KWA KIPINDI CHA JANUARI, 2017-
JANUARI, 2018**

[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2017 hadi Januari, 2018.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, Kamati inalaani vitendo vyote vya kihalifu vinavyohatarisha amani na usalama wa nchi ambavyo vinafanywa na wananchi wachache wasiopenda amani na utulivu katika Nchi yetu. Aidha, Kamati inawapa pole wananchi wote walioatharika na kuguswa na vitendo mbalimbali vya kihalifu kwa kipindi kinachotolewa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na kitendo cha kupigwa risasi Mbunge mwenzetu Mhe. Tundu A. Lissu, Mbunge wa Singida Mashariki, Mwezi Septemba, 2017, ambacho kilileta mshtuko mkubwa kwetu Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla. Watanzania wote tunapaswa kuendelea kulaani kitendo hicho. Kamati inaendelea kumuombea Mheshimiwa Tundu Lissu (Mb) kwa Mwenyezi Mungu amjalie uponyaji wa haraka na aweze kurudi katika hali yake ya kawaida na kulitumikia Taifa.

Aidha, Kamati inatoa pole kwa Watanzania na familia zote za Wanajeshi 15 waliopoteza maisha yao kishujaa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo walipokuwa wakihudumu katika Kikosi cha Umoja wa Mataifa cha kulinda Amani, mwezi Disemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Mwaka inawasilishwa tunapoelekea mwisho wa uhai wa Kamati katika nusu ya kwanza ya maisha ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 116 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Ninawashukuru Wajumbe wote Ishirini na Sita (26) wa Kamati ambao katika kipindi chote cha uhai wa Kamati wametumia Taaluma, Uzoefu na sifa nyingine muhimu katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Wajumbe hao ni wafuatao:-

1. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Kanal (Mst) Masoud Ali Khamis, Mb- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb- "
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb- "
5. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb- "
6. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb- "
7. Mhe. Victor Kilasile Mwambalaswa, Mb- "
8. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb- "
9. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb- "
10. Mhe. Cosato David Chumi, Mb- "
11. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb- "
12. Mhe. Bonnah Kaluwa, Mb- "
13. Mhe. Eng. Gerson Hosea Lwenge, Mb- "
14. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb- "
15. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb- "
16. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb- "
17. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb- "
18. Mhe. Lucy Simon Magereli, Mb- "

19. Mhe. Masoud Abdalla Salim, Mb-	"
20. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb-	"
21. Mhe. Stephen J. Masele, Mb-	"
22. Mhe. Machano Othman Said, Mb	"
23. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb-	"
24. Mhe. Khamis Yahya Machano, Mb-	"
25. Mhe. Yahya Omari Masare, Mb-	"
26. Mhe. Janeth Masaburi, Mb-	"

Aidha, naomba kuwatambua na kuwapongeza Mhe. George Huruma Mkuchika, Mb, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Kangi Aphaxad Lugola, Mb, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Mhe. Juliana Shonza, Mb, Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao walikuwa Wajumbe wa Kamati hii, kwa kuteuliwa katika nyadhifa hizo mwezi Novemba, 2017. Kamati inawatakiwa utekelezaji mwema wa majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii inaeleza shughuli zilizotekelizwa na Kamati kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018 na imegawanyika katika Sehemu Kuu nne zifuatazo:-

- i. Sehemu ya Kwanza inayotoa maeleo ya jumla kuhusu majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelizwa;
- ii. Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi na matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati;
- iii. Sehemu ya Tatu inayobainisha maoni na mapendekezo ya Kamati; na
- iv. Sehemu ya Nne ambayo ni hitimisho la taarifa hii.

1.2 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 6, Kifungu cha 3 pamoja na Fasili ya 7, Kifungu cha (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ni moja kati ya Kamati Tisa (9) za Kudumu za Bunge za Kisekta. Kamati hii inasimamia Wizara Tatu (3) ambazo ni:- Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, Majukumu ya Kamati hii ni yafuatayo:-

- i. Kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia;
- ii. Kushughulikia Miswada na Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia;
- iii. Kushughulikia Taarifa za Utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- iv. Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu ya kusimamia Wizara zilizoainishwa hapo juu, Kamati ina majukumu ya nyongeza matano (5) yaliyoainishwa kwenye Fasili ya 7, Kifungu cha 2, ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni yafuatayo:-

- i. Kuimarisha ushirikiano kati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge ya nchi nyingine;
- ii. Kufuatilia mwenendo na hali ya mtangamano wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika;
- iii. Kushughulikia taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika;
- iv. Kushughulikia taarifa zote za wawakilishi katika Vyama mbalimbali vya Kibunge ambapo Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama; na
- v. Kushughulikia Taarifa za hali ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka ya Nchi na Usalama wa Raia na Mali zao.

Mheshimiwa Spika, mbali na majukumu ya msingi ambayo yameorodheshwa hapo juu, Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Bunge imetoa ruhusa kwa Kamati yoyote ikiwemo Kamati hii, kupendekeza kwa Spika majukumu mengine ya nyongeza. Majukumu hayo ya nyongeza yanatekelezwa kwa namna mbili zifuatazo:-

- a) Kamati kupendekeza ipewe jukumu la nyongeza; na
- b) Mheshimiwa Spika kukabidhi Kamati jambo lingine lolote kadri atakavyoona inafaa kwa ajili ya kufanyiwa kazi na Kamati hiyo.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Septemba, 2017, Kamati ilikabidhiwa jambo moja na Mheshimiwa Spika la kushughulikia hali ya Ulinzi na Usalama nchini ikiwemo ulinzi wa Viongozi. Kamati ilitekeleza shughuli hiyo kwa ukamilifu na kuandaa Taarifa iliyotoa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ambayo Serikali inatakiwa kuyafanya kazi. Taarifa hiyo iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Spika kwa ajili ya utekelezaji wake.

1.3 Njia na Mbinu mbalimbali zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati ilitumia njia na mbinu mbalimbali zilizoendana na matakwa ya Kanuni ya 117 (3) (5) kuhusu kukutana na kuzingatia bajeti ya Kamati iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2016/2017 na 2017/2018. Njia zilizotumika ni:-

- i. Vikao na Wizara kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji za Wizara hizo pamoja na Taasisi zake;
- ii. Vikao na wawakilishi wa Vyama mbalimbali vya Kibunge kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Vyama hivyo;
- iii. Kuwataka Mawaziri kutoa maeleo na ufanuzi wa masuala mbalimbali yaliyohitaji ufanuzi;
- iv. Ziara za kuangalia na kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa masuala mbalimbali hususan Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara

- zinazosimamiwa na Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; na
- v. Kuwasilisha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti hoja mahsusizilizotokana na Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018; na

1.4 Shughuli zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2017 - Januari, 2018 Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetekeleza shughuli zifuatazo:-

1.4.1 Semina

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Februari, 2017 hadi Januari, 2018, Kamati ilishiriki na kuongoza Semina tatu zilizoandaliwa na Ofisi ya Bunge, chini ya Mradi wa Awamu ya Pili wa kuliwezesha Bunge unaodhaminiwa na UNDP.

Semina hizo zilihusu:-

- i) Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyofanyika tarehe 28 na 29 Oktoba, 2017;
- ii) Dhana na Utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau iliyofanyika tarehe 13 na 15 Septemba, 2017; na
- iii) Namna ya kuchambua Miswada ya Sheria na Udhibiti wa Sheria Ndogo katika Bunge la Tanzania iliyofanyika tarehe 04 na 05 Novemba, 2017.

1.4.2 Kupokea na Kujadili Taarifa za Utekelezaji za Wizara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia pamoja na Taasisi zake. Taarifa hizo zimeainishwa katika Kiambatisho namba 1.

Mheshimiwa Spika, lengo la kupokea na kujadili taarifa hizo ilikuwa ni kutekeleza jukumu la Kibunge la kuisimamia Serikali kama inavyotajwa katika Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Baada ya kujadili taarifa hizo kwa kina, Kamati ilibaini masuala mbalimbali ambayo yanafafanuliwa katika Sehemu ya Pili ya taarifa hii.

1.4.3 Kufuatilia utekekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuhusu Kamati za Kisikta kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia, Kamati hii ilikagua Miradi ya Maendeleo iliyo chini ya Wizara inazozisimamia ambayo ilitengewa fedha kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Jumla ya Miradi Nane (8) ilikaguliwa katika kipindi cha Mwezi Machi, 2017. Miradi hiyo pamoja na vifungu vyake ni ifuatayo:-

Fungu	Simbo ya Mradi	Jina la Mradi	Mahali ulipo	Thamani ya Mradi
14	6311	Ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi la zimamoto	Dar es Salaam	1,500,000,000.00
	6582	Ununuzi wa magari mawili ya Zimamoto		2,000,000,000.00
28	6107	<i>Offenders Management system na Digital mobile radio</i>	Dar es Salaam	100,000,000.00
	6302	Ufungaji wa lift katika jengo la Makao Makuu		300,000,000.00
34	6391 (411000)	Ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Ubalozi, Makazi ya Balozi na Mkuu wa Utawala	Maputo, Msumbiji	1,316,435,000.00

		Ukarabati wa Makazi ya Balozi na nyumba za Watumishi	Stockholm, Sweden	2,172,880,000.00
51	6501	Usajili na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa	Dar es Salaam	30,000,000,000.00
57	6103	Mikopo ya Mikataba ya ununuzi wa vifaa vya utafiti	Nyumbu, Pwani	177,500,000,000.00

Mheshimiwa Spika, mbali na kukagua Miradi iliyokuwa imetengewa fedha katika Mwaka 2016/2017, Kamati pia ilikagua majengo ya Ubalozi wa Tanzania yaliyoko katika Majiji ya Pretoria na Johannesburg nchini Afrika Kusini. Kamati ilifanya ziara hiyo ya ukaguzi kutokana na umuhimu wa ubalozi huo katika mahusiano ya Kiuchumi na Kidiplomasia kati ya nchi hiyo na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi uliofanywa, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yalioathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Masuala hayo yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya Pili ya taarifa hii.

1.4.4 Kuchambua Taarifa za Wizara kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Nane, Kifungu cha 7(1) (a) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa ajili ya kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchambuzi uliofanywa na Kamati yanaelezwa kwa kina katika sehemu ya pili ya Taarifa hii.

1.4.5 Kuchambua Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati hii ilishughulikia Mikataba miwili ya Kimataifa ifuatayo:-

- i) Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula (The East African Community Protocol on Sanitary and phytosanitary Measures); na
- ii) Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (The East African Community Protocol on Peace and Security)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa kina Itifaki hizo na kuwasilisha Bungeni Maoni na Ushauri wake kuhusu Itifaki ya Amani na Usalama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati haikuwasilisha maoni na ushauri kuhusu Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Afya ya Mimea, Usalama wa Wanyama na Chakula kwa kuwa ilibainika kuwa na changamoto kadhaa ambazo Serikali iliomba muda zaidi wa kuzishughulikia.

1.4.6 Mapitio ya Taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, moja ya majukumu ya Kamati hii ni kushughulikia taarifa za Wawakilishi wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge; na katika Bunge la Afrika Mashariki, SADC na Bunge la Afrika. Jukumu hili limeainishwa katika Kifungu cha 7 (2) (iii & iv) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Januari 2017- Januari, 2018, Kamati ilifanya mapitio ya taarifa za Wawakilishi wa Bunge katika SADC - PF, CPA na ACP/EU.

Taarifa zilizopitiwa ni zifuatazo:-

- i) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola (CPA);
- ii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Bunge la Pamoja la Nchi za *Africa, Caribbean na Pacific* (ACP) na Umoja wa Ulaya (ACP/EU); na
- iii) Taarifa ya Wawakilishi wa Bunge katika Jukwaa la Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC- PF).

Nakala za taarifa za wawakilishi wa Mabunge na Vyama hivyo zimeambatishwa katika Taarifa hii (Viambatisho 2-4).

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

2.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, baada ya kuainisha majukumu ya Kamati na shughuli zilizotekelawa kwa kipindi cha Januari 2017 hadi Januari, 2018, sasa naomba kutoa taarifa kuhusu masuala mbalimbali yaliyobainika wakati Kamati ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, masuala yatakayotolewa taarifa ni yale ambayo Kamati imebaini kuwa changamoto zake zinahitaji kupewa umuhimu wa kipekee ili kuziwezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hivyo kuleta tija kwa Taifa. Masuala hayo ni:-

a) Masuala ya Ujumla

Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- i) Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi;
- ii) Ajali za Barabarani;
- iii) Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao;
- iv) Udhibiti na usalama wa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wabunge;
- v) Msongamano wa mahabusu na wafungwa katika magereza;
- vi) Utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto;
- vii) Huduma za Wakimbizi nchini; na
- viii) Utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uhamiaji.

c) Wizara ya Ulinzi na JKT

- i) Kukosekana kwa Sera ya Taifa ya Ulinzi;
- ii) Kukosekana kwa alama za Mipaka ya Nchi;
- iii) Ubovu wa barabara za Mipakani;

- iv) Utendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT);
- v) Migogoro ya ardhi katika Jeshi la Kujenga Taifa;
- vi) Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria; na
- vii) Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC).

d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

- i) Utendaji wa *African Peer Review Mechanism* (APRM);
- ii) Utendaji wa Chuo cha Diplomasia;
- iii) Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC);
- iv) Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC);
- v) Balozi za Tanzania kutopata fedha za miradi kwa wakati;
- vi) Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania;
- vii) Hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- viii) Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje; na
- ix) Mawasilisho ya Maazimio ya Bunge.

e) Uwakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

Ushiriki wa Wawakilishi wa Tanzania katika Mabunge mengine na Vyama mbalimbali vya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutoa maeleo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kwenye masuala yaliyoainishwa hapo juu katika sehemu ya taarifa inayofuata.

2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Kamati

2.2.1 Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofanya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2016/2017 ilibaini kuwa ucheleweshwaji au kutokupatikana kabisa kwa fedha kutoka Hazina na wakati mwingine kutoka kwenye Wizara Mama, ilikuwa ni changamoto katika utekelezaji wa miradi iliyotembelewa. Kutokana na

changamoto hiyo, Kamati ilibaini kuwa utekelezaji wa miradi uligawanyika katika makundi matatu.

Mheshimiwa Spika, kundi la kwanza ni miradi ambayo haikutekelezwa kabisa kutokana na kutokupelekewa fedha. Taarifa mbalimbali zilizotolewa mbele ya Kamati zilionesha kuwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo hazikutolewa kabisa, jambo lilokwamisha utekelezaji wake. Mfano wa Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6311** kuhusu ukamilishaji wa Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Zimamoto uliotengewa Shilingi Bilioni 2. Mfano mwagine ni **Mradi Na. 6302** kuhusu ufungaji wa lift katika jengo la Makao Makuu ya Jeshi la Polisi uliotengewa Shilingi Milioni 300.

Mheshimiwa Spika, kundi la Pili ni miradi ambayo ilitekelezwa kwa sehemu kutokana na kupelekewa fedha pungufu ikilinganishwa na kiasi kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mfano wa Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6103** kuhusu malipo ya Mikopo ya Ununuzi wa vifaa vya Utafiti katika Shirika la Nyumbu.

Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Mradi huu ulitengewa Shilingi Bilioni 151.1 kwa ajili ya kulipa madeni ya Mikataba ya ununuzi wa vifaa vya utafiti. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi 2017, mradi huu ulikuwa umepokea Shilingi Bilioni 30 ikiwa ni asilimia 20 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kutokutolewa kwa fedha hizi kwa ukamilifu kuliathiri ratiba za malipo ya Mikataba hiyo na hivyo kuzalisha madeni ya kimkataba na riba.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni miradi ambayo haikupelekewa fedha za utekelezaji wake kutoka Wizara mama. Mfano wa Mradi huo ni **Mradi Na. 6391** kuhusu Ukarabati wa Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi Jijini Stockholm nchini Sweden. Maeleo yaliyotolewa na Ubalozi mwezi Mei, 2017 yalibainisha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 2,172,880,000/=. Kamati ilibaini kuwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilipokea fedha hizo kutoka Hazina tarehe 2/12/2016. Hata hivyo,

hadi Kamati inakagua mradi huo Mwezi Mei, 2017, fedha hizo zilikuwa hazijawasilishwa. Kamati iliarifiwa baadae kuwa fedha hizo ziliwasilishwa katika Ubalozi wa Sweden tarehe 07/06/2017.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hazikupokea kwa ukamilifu fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Taswira ya mtiririko wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo unaonekana katika Jedwali namba. 1

Jedwali Na. 1: Hali ya upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Wizara	Bajeti iliyoidhinishwa	Fedha zilizopokelewa	% ya fedha zilizotolewa	% ya fedha isiyotolewa
Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki	8,000,000,000	3,489,315,000	43.6	56.4
Ulinzi na JKT	248,000,000,000	35,900,000,000	14.5	85.5
Mambo ya Ndani ya Nchi	47,923,421,105	13,466,336,364	28	72
JUMLA	303,923,421,105	52,855,651,364	17	83

Chanzo:- Randama za Wizara husika 2017/2018

2.2.2 Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Polisi

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2002, likiwa na Jukumu la kulinda amani na utulivu, kubaini, kupeleleza na kuzuia uhalifu, kuwakamata wahalifu na kuwaweka chini ya ulinzi, kulinda mali na kusimamia utekelezaji wa Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Jeshi hilo kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2017. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini kuwa Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza majukumu yake likiwa na changamoto mbalimbali kama vile upungufu wa vitendea kazi kama vile magari, na upungufu wa mafuta na vilainishi kwa ajili ya magari machache yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Changamoto hizo zinasababishwa na kutopatikana kwa ukamilifu kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya Jeshi hilo. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Jeshi la Polisi lilitengewa Shilingi Bilioni 247,111,051,682/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi Bilioni 5,000,000,000-= kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2017 Jeshi lilipokea Shilingi Bilioni 124,637,484,397/= sawa na asilimia 50 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na Shilingi Milioni 193,000,000/= za Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 3.9 tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, kutopatikana kwa fedha kwa ukamilifu kumeathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa katika kipindi hicho hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu nchini, upelegezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za Baharini na Maziwa Makuu.

2.2.3 Ajali za Barabarani

Mheshimiwa Spika, makosa yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria za usalama barabarani yameendelea kusababisha ajali za barabarani nchini. Kwa kipindi cha Oktoba - Disemba, 2017 jumla ya ajali 1428 ziliripotiwa ambapo kati ya hizo, ajali 562 zilisababisha vifo.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Wizara ilionesha kuwa vifo hivi ni pungufu ya ajali 91 zilizosababisha vifo ikilinganishwa na idadi ya vifo vya aina hiyo katika kipindi kama hicho Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudzi za Jeshi la Polisi hususan kitengo cha Usalama Barabarani kwa kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani ipasavyo. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali itekeleze ushauri uliotolewa na Kamati katika taarifa yake ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017 kuhusu kufanya marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973, ili iguse maeneo sita yenye mapungufu ambayo yanachangia ajali za barabarani zinazosababisha vifo. Maeneo hayo ni:-

- i) Mwendokasi;
- ii) Uvaaji wa kofia ngumu;
- iii) Ufungaji wa mikanda;
- iv) Matumizi ya kilevi;
- v) Matumizi ya simu za mkononi; na
- vi) Matumizi ya vizuizi vya Watoto.

2.2.4 Ulinzi na usalama wa Raia na mali zao

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa, Kamati ilikutana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa vipindi tofauti vya Mwezi Septemba, 2017 na Januari, 2018 kwa lengo la kupokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Usalama wa Raia na mali zao. Taarifa hizo, pamoja na mambo mengine, zilibainisha hali ya uhalifu nchini na matukio yanayohatarisha hali ya usalama wa Raia na mali zao nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhishwa na juhudzi za Serikali katika kushughulikia matukio mbalimbali ya uhalifu hususan matukio ya Kibiti, Mkuranga na Rufiji ambayo yalihusisha mauaji ya Viongozi mbalimbali, Askari Polisi na Raia. Nafurahi kutoa taarifa kuwa, kwa kazi nzuri iliyofanywa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika maeneo hayo, hali ya usalama sasa ni shwari. Hata hivyo, Kamati inasisitiza kuwa ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kiini cha mauaji hayo kinajulikana na kudhibitiwa ili mauaji ya aina hiyo yasijirudie tena nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Jeshi la Polisi katika kudhibiti uhalifu nchini, Kamati ilibaini kuwa kumekuwa na ucheleweshwaji wa kutoa taarifa rasmi kwa Umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu na yanayovuta hisia za Jamii kama vile matukio ya mauaji, kutekwa na kupotea kwa Viongozi na Wananchi mbalimbali, unyang'anyi wa kutumia silaha na makosa makubwa ya uhujumu uchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilibaini kuwa baadhi ya Wakuu wa Wilaya wanawaweka mahabusu Wananchi na Watumishi wa Umma kinyume cha matakwa ya Kifungu cha 15 cha Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 1997. Ni wajibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na TAMISEMI kuendelea kuwaelimisha Wakuu wa Wilaya kuhusu matumizi sahihi ya Sheria hiyo ingawa kwa sasa vitendo hivyo vimepungua.

2.2.5 Udhibiti wa Usalama wa Viongozi wa Serikali wakiwemo Wabunge

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwezi Novemba, 2017 Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Udhibiti wa Usalama wa Viongozi wakiwemo Wabunge. Kamati ilichambua na kujadili Taarifa hiyo ambapo ilibainika kuwa Viongozi wanaolindwa na Jeshi la Polisi kwa Mujibu wa Sheria ni wafuatao:-

- i) Viongozi Wakuu wa Nchi ambao ni Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Waziri Mkuu na Viongozi Wakuu Wastaifu;
- ii) Viongozi waandamizi wa Serikali ambao ni Mawaziri na Manaibu Mawaziri;
- iii) Wakuu wa Mikoa na Wilaya;na
- iv) Spika na Naibu Spika wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi Sura ya 322, Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hupewa ulinzi wa

jumla wanapokuwa Bungeni au kwenye safari zao za kikazi. Utaratibu huu unaliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge katika makazi yao wakiwa kwenye shughuli za Bunge na kwenye maeneo yao ya uwakilishi kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe.

2.2.6 Msongamano wa wafungwa katika Magereza

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Jeshi la Magereza kwa kipindi cha Januari - Septemba, 2017, ilibaini kuendelea kuwepo kwa tatizo sugu la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza nchini.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ulionesha kuwa hali hii imeendelea kuchangiwa na:-

- i) Uchache wa magereza nchini ikilinganishwa na idadi ya wafungwa;
- ii) Utegemezi wa adhabu ya kifungo Gerezani na matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na huduma kwa Jamii;
- iii) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *parole*;
- iv) Wahamiaji haramu wanaokamatwa kwa makosa ya kuingia nchini isivyo halali kukaa magerezani kwa muda mrefu;
- v) Kasi ndogo ya kusikiliza mashauri yanayohusu mauaji na dawa za kulevy;a;na
- vi) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msongamano wa wafungwa, Kamati ilibaini changamoto nyingine mbalimbali zinazolikabili Jeshi la Magereza katika kutekeleza majukumu yake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i. Upungufu wa Watumishi takribani 11,395;

- ii. Ufinyu wa Bajeti na hivyo kulifanya Jeshi hilo kushindwa kujenga nyumba za Watumishi zinazolingana na mahitaji ya Jeshi, kushindwa kununua vitendea kazi kama vile magari na sare za Watumishi na wafungwa, kukarabati majengo ya Ofisi za Magereza, na kushindwa kupima maeneo ya Jeshi hivyo kusababisha migogoro ya ardhi na Jamii inayoizunguka kama vile katika magereza ya King'ang'a - Dodoma, Morogoro Mjini, Namajani- Mtwara na Mollo- Rukwa.

2.2.7 Utekelezaji wa majukumu ya Kikosi cha Zimamoto

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa Taarifa hii, Kamati ilibaini kuwa Serikali imeendelea kutolipa Jeshi la Zimamoto uzito unaostahili kwa kuzingatia majukumu ya Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, Mwezi Mei, 2017 Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali kuhusu kutoa kwa ukamilifu Shilingi Bilioni 3.5 za Miradi ya Maendeleo ya Jeshi hilo. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 2 ziliidhinishwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Makao Makuu yake uliokwama tangu Mwaka 2013, na Shilingi Bilioni 1.5 zilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kuzimia moto.

Hata hivyo, ilibainika kuwa, hadi kufikia Mwezi Juni, 2017, Serikali kuitia Hazina ilitoa Shilingi 117,045,000/= tu za Miradi ya Maendeleo licha ya kuwa katika Mwaka huo wa fedha Kikosi hicho kilikusanya Shilingi 31,725,254,500/=. Kutokutolewa kwa fedha hizo kumeathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo zinazohusiana na Mifumo na juhudzi za uokoaji na zimamoto.

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto ya upatikanaji wa fedha za maendeleo, Kikosi hicho kimeendelea kukabiliwa na uhaba wa dawa za kuzimia moto na uchakavu wa magari ya kuzimia moto na uokoaji jambo linalozorotesha utaratibu na juhudzi za zimamoto na uokoaji.

2.2.8 Huduma za Wakimbizi Nchini

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wakimbizi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), imeendelea kutoa huduma mbalimbali kwa Wakimbizi nchini kwa kuzingatia Sheria Namba 9 ya Wakimbizi ya Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Wakimbizi ya Mwaka 2003 na Mikataba mbalimbali ambayo nchi yetu imeridhia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya kuwahudumia wakimbizi kwa kipindi cha Januari- Septemba, 2017. Taarifa hiyo ilionesha kuwa Tanzania ni mionganii mwa nchi 11 zilizopendekezwa kutekeleza Mpango jumuishi wa Umoja wa Mataifa ujulikanao kama '*Comprehensive Refugee Response Framework*'. Mpango huu utawasaidia wakimbizi pamoja na Jamii wenyeji katika maeneo ambayo wakimbizi wanahifadhiwa kunufaika na miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Umoja wa Mataifa, Kamati ilibaini kuwa bado upo umuhimu wa Serikali yetu kuendelea kutafuta suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi hapa nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta suluhu za kudumu katika nchi zenyet machafuko, kuwahamishia wakimbizi katika nchi ya tatu, kuwapa uraia na kuwatawanya katika maeneo mbalimbali nchini.

2.2.9 Idara ya Uhamiaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai 2016 hadi Juni, 2017, Idara ya Uhamiaji ilipanga kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwemo kutoa huduma ya pasipoti na hati za dharura za safari kwa watanzania wanaosafiri nje ya nchi, na ununuzi wa mafuta ya magari kwa ajili ya doria na matumizi mengine ya Idara.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Idara ya Uhamiaji kwa kipindi tajwa, Kamati ilibaini kuwa uhaba wa fedha uliathiri utekelezaji wa shughuli zilizokuwa zimepangwa ikiwemo Idara kushindwa

kufanya misako na doria ya mara kwa mara kwa kutokua na vitendea kazi kama vile magari na uhaba wa mafuta.

Aidha, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Idara inakabiliwa na madeni makubwa ya wazabuni ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu kuanzia Mwaka 2013/2014 hadi 2016/2017 yanayofikia kiasi cha Shilingi Bilioni 10,291,374,513.46. Jambo hili limesababisha Idara kushindwa kupata huduma kwa wakati ikiwemo upatikanaji wa vitabu vya Pasipoti na malighafi zake.

2.2.10 Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kuishauri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuharakisha Mchakato wa kuhuisha Sera ya Taifa ya Ulinzi (The National Defence Policy) tangu Kamati hii ilipoanza kutekeleza majukumu yake Mwezi Januari, 2016. Ushauri huu ni mwendelezo wa jitihada za iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika Bunge la Tisa na Bunge la Kumi katika kuisisitiza Serikali kuona umuhimu wa kuwa na Sera ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, katika vikao vya Kamati vya Mwezi Oktoba, 2017, Kamati ilielezwa kuwa mchakato huo bado unaendelea. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa mchakato wa Sera hiyo bado haujakamilika. Jambo hili linaathiri utekelezaji wa masuala mengine ya msingi yanayotegemea uwepo wa Sera hiyo kama vile maboresho ya fidia kwa Askari wanaoumia au kufariki wakiwa kazini.

2.2.11 Alama za Mipaka ya Nchi (Beacons)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa kuhusu Hali ya Mipaka ya Nchi Mwezi Oktoba, 2017, ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto ya kukosekana kwa alama za Mipaka (Beacons), na uwepo wa makazi na shughuli za Kilimo na Ufugaji katika maeneo ya Mipaka ambayo hayaruhusiwi kisheria.

Kumbukumbu zinaonesha kuwa changamoto hii ni ya muda mrefu na imekuwa ikiripotiwa Bungeni tangu Bunge la Nane. Ni wazi kuwa tatizo hili lisiposhughulikiwa litahatarisha usalama wa Taifa.

2.2.12 Barabara za Mipakani

Mheshimiwa Spika, ubovu wa barabara za mipakani umeendelea kusababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka yetu kwa nyakati zote. Mwezi Disemba, 2013, iliyokuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ya Bunge la Kumi iliishauri Serikali kuhusu changamoto hiyo, Nanukuu:

‘Ofisi ya Waziri Mkuu kuhakikisha kwamba suala la ujenzi na ukarabati wa barabara za usalama mipakani linawekewa mkakati maalumu wa kitaifa. Moja ya mikakati hiyo iwe ni kuziweka barabara hizi chini ya TANROADS, na tenda za matengenezo zitolewe kwa vitengo vya uhandisi vya Jeshi na JKT kwa vile wana wataalamu na zana za kutengeneza barabara’¹

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hadi sasa ikiwa ni Miaka Mitano (5) tangu ushauri huo utolewe jambo hilo bado halijatekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha.

2.2.13 Shirika la SUMA JKT

Mheshimiwa Spika, Shirika la uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa Mwaka 1982 kwa Sheria ya Makampuni namba 23 ya Mwaka 1974. Jukumu kuu la Shirika hili ni kuchochaea shughuli za uzalishaji mali ili kusaidia gharama za malezi ya Vijana wanaopitia JKT.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili taarifa ya Utendaji wa Shirika la SUMA JKT mwezi Oktoba, 2017, ilibaini kuwa Kampuni ya SUMAJKT GUARD inakabiliwa na changamoto ya muda mrefu ya madeni kutoka kwa washitiri ambapo gharama kubwa hutumika katika kufuatilia madeni hayo. Aidha, Kamati

¹ Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Shughuli zake kwa kuanzia Machi hadi Novemba, 2013

ilibaini kuwa, mradi wa matrekta na Zana za Kilimo (Agrimachinery) una changamoto ya urejeshwaji wa madeni kutoka kwa Wakulima, Halmashauri za Wilaya na Viongozi waliokopa matrekta. Hadi taarifa hiyo ilipokuwa inawasilishwa mbele ya Kamati, madeni hayo yalikuwa takribani Shilingi Bilioni 40.

Mheshimiwa Spika, madeni haya kwa Mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri utendaji wa Shirika hilo hususan katika kutimiza jukumu lake la kuchochea shughuli za uzalishaji mali kwa lengo la kusaidia gharama za malezi ya Vijana wanaopita JKT.

2.2.14 Migogoro ya Ardhi katika JKT

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikijadili taarifa ya utekelezaji wa JKT ilibaini kuwepo kwa migogoro ya ardhi katika baadhi ya Vikosi vya Jeshi hilo. Migogoro hiyo inasababishwa na kuwepo kwa wavamizi wa ardhi ya Jeshi ambao hawataki kuhama katika maeneo hayo na Wananchi kutokulipwa fidia kwa maeneo yaliyochukuliwa kwa matumizi ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa wakati uvamizi katika maeneo ya Jeshi unachangiwa na ongezeko la idadi ya watu na mahitaji makubwa ya ardhi, Wananchi kutolipwa fidia kunasababishwa na kutokutolewa kwa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya suala hilo.

2.2.15 Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria kwa Vijana wanaohitimu Elimu ya Sekondari yalirejeshwa Mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na mihula ya kumaliza Kidato cha Sita kutoendana na muda wa Vijana kujiunga na mafunzo ya JKT, Vijana hao hulazimika kupata mafunzo hayo kwa miezi Mitatu tu badala ya Mwaka Mmoja. Kamati inaona kuwa muda huo ni mchache kuwajengea moyo wa uzalendo Vijana vilevile kuwaandaa kuwa Jeshi la Akiba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kurudisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, Kamati imebaini kuwa bado Serikali hajjalipa kipaumbele Jeshi hilo katika kuboresha miundombinu yake. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, JKT lilitengewa jumla ya Shilingi Biloni 8 ikiwa ni fedha za maendeleo kwa ajili ya shughuli za ujenzi na ukarabati vikosini. Hadi kufikia Mwezi Juni, 2017 fedha iliyokuwa imetolewa ni Shilingi Bilioni 1 sawa na asilimia 12.5 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, JKT limetengewa Shilingi Bilioni 6 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo hadi kufikia Mwezi Januari 2018, fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

2.2.16 Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Ulinzi (National Defence College) kilianza rasmi Mwaka 2012. Chuo hiki maalum kimejikita katika kutoa mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa Maafisa Waandamizi kutoka Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Vyombo vyta Usalama, Watumishi wa juu wa Serikali pamoja na Maafisa Waandamizi kutoka majeshi ya nchi rafiki za Afrika na nje ya Afrika. Lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea washiriki wa kozi maarifa katika Nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijeshi, kisayansi, mahusiano ya kimataifa na kuwaongeza weledi wa uongozi kwa kiwango cha kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya NDC, ilibaini kuwa, uchache wa vyumba vyta kulala, vyumba vyta kuendeshea Semina na majadiliano ni changamoto inayokikabili Chuo. Changamoto hii imesababisha Chuo kuchukua washiriki wachache tofauti na idadi iliyokusudiwa na vilevile kushindwa kuendesha Kozi ndefu na fupi kwa wakati mmoja. Hata hivyo, Kamati inapongeza juhudzi za Serikali katika kutatua changamoto hiyo ambapo maandalizi yote ya ujenzi wa jengo jipya la Chuo (awamu ya pili) yameshakamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini upatikanaji wa washiriki hususan kutoka katika Wizara mbalimbali ni changamoto nyingine ya Chuo hicho. Jambo hili

linasababishwa na baadhi ya Wizara kutopeleka washiriki katika mafunzo hayo muhimu kwa Maafisa Waandamizi kwa kigezo cha uhaba wa fedha. Kamati inaamini mafunzo haya ni muhimu hivyo Wizara zote zinatakiwa kupeleka Maafisa Waandamizi kama ambavyo Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimekuwa vikifanya.

Mheshimiwa Spika, ipo haja ya Serikali kuandaa utaratibu wa kuwafanya Maafisa waandamizi wa Wizara zote kushiriki Mafunzo hayo muhimu. Aidha, upo umuhimu wa Wabunge kupewa mafunzo ya usalama na stratejia yanayotolewa na Chuo hicho.

2.2.17 Utekelezaji wa Shughuli za Mpango wa Tathmini ya Utawala Bora (APRM Tanzania)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mionganoni mwa nchi 36 kati ya 54 za Umoja wa Afrika zilizojiunga na Mpango huu wenyewe lengo la kuzisaidia Serikali za Afrika, ikiwemo Tanzania, kuimarisha Utawala Bora kwa kuwashirikisha Wananchi kubaini changamoto za kufanyiwa kazi na mambo mazuri ya kuigwa na kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea taarifa ya utendaji ya APRM Tanzania, ilielezwa kuwa changamoto kubwa inayoikabili Taasisi hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake ni mgao mdogo wa fedha za Bajeti zinazopangwa. Hali hiyo imesababisha Taasisi hiyo, pamoja na mambo mengine, kushindwa kutekeleza kikamilifu Mkakati wa mawasiliano unaolenga kuendelea kuhamasisha Umma kuhusu APRM na hivyo kutofahamika vema kwa Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa nguzo muhimu ya Mpango wa APRM ni ushirikishwaji mpana wa Wananchi ili kupata maoni kutoka kwa Wadau wote muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Kamati, kwa kipindi cha miaka takribani mitano mfululizo, imekuwa ikiishauri Serikali kuipatia APRM Fungu lake la kibajeti, ushauri ambao haujatekelezwa.

2.2.18 Utendaji wa Chuo cha Diplomasia

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam kilianzishwa mwaka 1978 kwa ushirikiano wa nchi mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Msumbiji. Tangu kuanzishwa kwake, Chuo hiki kimeendelea kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika Nyanja za mahusiano ya Kimataifa, Diplomasia, Diplomasia ya Uchumi, Itifaki, Lugha za Kigeni na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kwa takribani Miaka 36 Chuo hiki kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kuacha kabisa kuchangia bajeti na kushiriki katika shughuli zote za uendeshaji wake Mwaka 1982. Suala hili limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Chuo na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo imeendelea kubeba jukumu la kukiendesha na kugharamia shughuli zote za Chuo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto iliyoelezwa hapo juu, Kamati ilibaini kuwa Chuo kimekuwa na changamoto nyingine ya kutimiza na kutekeleza viwango vilivyowekwa na NACTE kutokana na ukosefu wa pesa za kutosha. Viwango hivyo ni pamoja na:-

- i) Kuwa na wataalamu wenye vigezo vinavyotambulika;
- ii) Kuboresha majengo na Miundombinu ya Kitaalamu;
- iii) Matumizi ya teknolojia katika Taaluma na Utawala.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa changamoto hii isipopewa uzito unaostahili inaweza kusababisha Chuo hicho kufutiwa usajili wa NACTE.

2.2.19 Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC)

Mheshimiwa Spika, Dhana ya Diplomasia ya Mikutano (Conference Diplomacy) inatambua Vituo vya Mikutano vya Kimataifa kutumika kutangaza nchi zao Kimataifa kwa ajili ya ujio wa wageni katika vituo hivyo. Kwa sababu hiyo, nchi nyingi mbalimbali zimekuwa na utaratibu wa kuwekeza kwenye vituo vya Mikutano ya Kimatifa kwa ajili ya Utalii wa Mikutano. Kwa upande wa Tanzania, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kimekuwa sababu ya vivutio vya Utalii katika mzunguko wa Kaskazini kupata Watalii wengi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha kilanza rasmi Mwaka 1978 kufuatia kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuia ya Afrika Mashariki Mwaka 1977. Katika kutekeleza shughuli zake, Kituo kinachukua sura ya kuitangaza Tanzania katika Utalii wa Mikutano na matukio (business tourism) na hivyo kuchangia katika pato la Taifa kupitia Sekta ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wake muhimu katika Sekta ya Utalii, Kituo hicho kinakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

- i) Matumizi ya majengo ambayo hayakujengwa rasmi kwa shughuli za mikutano;
- ii) Ukiritimba katika kupata Hati Miliki za baadhi ya viwanja vyake;
- iii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kwa ajili ya kuitangaza nchi, kuvutia Mikutano na maonesho ya Kimataifa kufanyika nchini; na
- iv) Utata wa umiliki wa Kiwanja Na. 45 eneo la corridor 1 kuwa cha ESAMI au AICC

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza wazo la AICC la kuwa na tawi lake katika Makao Makuu ya Nchi Mjini Dodoma. Ni vema Wizara ikafuatilia kwa karibu maombi ya kupatiwa Kiwanja cha kujenga Kituo cha kisasa cha Mikutano cha Kimatifa kitakachokuwa na eneo la kutosha kwa ajili Mikutano, maonesho na

Hoteli za kisasa. Aidha, kwa siku za usoni, Kituo kiwe na mpango wa kufungua tawi lake Zanzibar, ambako kuna fursa nyingi za kitalii.

2.2.20 Utendaji wa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC)

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere kinasimamiwa na Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) tangu Aprili, 2014. Dhima ya kituo hiki ni kukuza na kutoa huduma bora za Utalii wa Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya kukuza maendeleo ya Taifa kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kimekuwa na mafanikio mbalimbali tangu kilipoanzishwa. Moja ya mafanikio hayo ni kuongezeka kwa mapato² kutokana na shughuli za mikutano ambazo ndio hasa zinazotangaza Kituo, Jiji la Dar es Salaam na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio ya Kituo hicho, Kamati ilibaini kuwa JNIC inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri utekelezaji wake. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i) Kutokuwepo kwa eneo la maonesho;
- ii) Kutokuwepo kwa eneo la chakula kwa wageni wa mikutano;
- iii) Kutokuwa na Hati Miliki ya Kiwanja chake;na
- iv) Ubovu wa miundombinu ya maji, majitaka, umeme na viyoyozi.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikashughulikia changamoto hizo ili Kituo hicho kiweze kutoa huduma bora zaidi za Utalii wa Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa. Aidha, Serikali iwe makini inapopewa misaada inayohusu ujenzi wa majengo kwa kuhakikisha kuwa majengo yanayojengwa yanakidhi vigezo.

² Mapato yameongezeka kutoka Sh. 2,023,350 Mwaka 2013/2014 hadi kufikia 2,738,009 Mwaka 2016/2017

2.2.21 Balozi za Tanzania kutopata fedha kwa wakati

Mheshimiwa Spika, Balozi zetu zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya kutopata fedha kwa wakati jambo ambalo linaathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo. Licha ya ushauri unaotolewa na Kamati hii mara kwa mara kuhusu utaratibu wa Hazina kupeleka fedha moja kwa moja kwenye Balozi hizo badala ya kupeleka Wizarani, bado ushauri huo haujatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofanya ziara katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden na Msumbiji ilibaini kuwa Balozi hizo zimeendelea kupelekewa fedha kutoka Wizarani na si Hazina, jambo ambalo linasababisha fedha hizo kuchelewa kutumwa. Hali hii imeathiri utekelezaji wa majukumu ya Balozi hizo ikiwa ni pamoja na gharama za utekelezaji wa mradi uliopo Maputo kuongezeka hadi kufikia USD 3,056,839.15 kutoka gharama za awali za USD 2,107,028.89 wakati Mkataba wa utekelezaji uliposainiwa Mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa Serikali bado haijaupa ushauri huo uzito unaostahili kwani upatikanaji wa fedha katika Balozi nyingi umeendelea kuwa katika mtiririko usio wa kuridhisha.

2.2.22 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania

Mheshimiwa Spika, majengo ya baadhi ya Balozi zetu yameendelea kuwa chakavu kutohana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu. Kamati hii ilipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi wa ukarabati wa majengo katika Ubalozi wa Tanzania nchini Sweden Mwezi Mei, 2017, ilishuhudia uchakavu uliokithiri wa majengo ya Makazi ya Balozi na Nyumba za Watumishi wa Ubalozi huo. Aidha, Kamati ilibaini kuwa, majengo hayo hayajafanyiwa ukarabati kwa takribani Miaka Tisa.

Mheshimiwa Spika, uchakavu wa majengo ya Balozi unasababisha athari mbalimbali kwa Taifa letu. Athari hizo ni pamoja na:-

- i) Kuliondolea Taifa heshima na kuharibu taswira ya Tanzania nje ya nchi;
- ii) Serikali kulipa gharama kubwa kwa ajili ya Kodi ya Pango ya nyumba za makazi kwa Mabalozi na Watumishi wa Ubalozi; na
- iii) Kuondolewa kwa kinga ya ubalozi kwenye majengo hayo.

2.2.23 Hali ya Ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kujadili taarifa ya hali ya ushirikiano wa Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki ilibaini kuwa, pamoja na faida zinazopatiana ndani ya Jumuiya za Kikanda na Mtangamano wa Afrika Mashariki, zipo changamoto mbalimbali ambazo zisiposhughulikiwa zinaweza kuathiri hali ya Ushirikiano na Mtangamano uliopo. Changamoto hizo ni pamoja na:-

- i. Kasi Ndogo ya kuridhia Itifaki mbalimbali za SADC kwa nchi Wanachama. Kati ya Itifaki 31 za SADC, Tanzania imesaini Itifaki 28 na kuridhia 25;
- ii. Migogoro ya kisiasa ndani ya nchi Wanachama wa SADC kama vile Lesotho, Madagascar na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo; na
- iii. Kuwepo na vikwazo mbalimbali visivyo vya kiushuru mionganini mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vikwazo hivyo vinadhoofisha ufanyaji wa biashara baina ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika kikao hicho Kamati ilihoji na kubaini kuwa bado Serikali haina Sera mahsusini inayotoa mwongozo kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki, licha ya kwamba suala hili limekuwa likishauriwa tangu Bunge la Tisa na Serikali kutoa maelezo kuwa mchakato wa uandaaji wa Sera hiyo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kuwa jambo hili halijapewa uzito unaostahili na Serikali kwani Tanzania imekuwa Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa takribani Miaka Kumi na Nane na mpaka sasa hakuna Sera

hiyo muhimu. Ni lazima Serikali itambue kuwa ipo hatari ya kutekeleza jambo lisilokuwa na mwongozo bora wa kisera.

2.2.24 Utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje (2001) inayoweka msisitizo katika kukuza uchumi wa nchi kupitia Diplomasia ya Uchumi iliyo endelevu. Hata hivyo Sera hiyo tangu iundwe mwaka 2001, imeendelea kutumika bila kufanyiwa marekebisho yanayozingatia mabadiliko ya sasa ya Kiuchumi, Kisiasa, Kijamii na mazingira yanayotokea duniani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipowasilisha taarifa yake ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017, ilishauri Mchakato wa marekebisho wa Sera hiyo uharakishwe ili iendane na mazingira ya sasa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kasi ya mchakato wa marekebisho ya Sera hiyo bado hairidhishi.

2.2.25 Meli za Nchi za Nje zilizopewa Usajili Tanzania

Mheshimiwa Spika, Siku za karibuni imejitokeza changamoto ya baadhi ya Meli zilizopewa usajili Tanzania kukamatwa zikifanya vitendo vya kihalifu ikiwemo kubeba madawa ya kulevyta na vifaa vya kutengenezea silaha kali za kivita. Jambo hilo limeitia aibu nchi yetu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa.

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kama ilivyoahidi Bungeni tarehe 02/05/2017 na kusawazisha kasoro za msingi zilizosababisha jambo hili ili lisitokee tena.

2.2.26 Kuwasilisha Maoni kuhusu Azimio la Bunge

Mheshimiwa Spika, katika Kikao cha Tatu cha Mkutano wa Nane wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliwasilisha Bungeni maoni na ushauri kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Amani na Usalama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Protocol on Peace and

Security). Lengo la Itifaki hii ni kuimarisha amani, usalama na utulivu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na kukuza ujirani mwema kwa nchi wanachama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokuwa ikifanya uchambuzi wake, ilibaini kuwa Itifaki hiyo ilisainiwa na nchi Wanachama tarehe 15 Februari, 2013. Hivyo, Itifaki hii ilichukua Miaka Minne hadi ilipoletwa Bunge kwa ajili ya kuridhiwa licha ya kuonekana kuwa ina manufaa makubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Ni vyema Serikali ikashughulikia dosari zote za aina hii kwa kuwasilisha Itifaki zote zilizosainiwa ambazo zinahitaji kuridhiwa na Bunge ili zirimhiwe na utekelezaji wake uanze mara moja kwa kuzingatia matakwa ya Sheria. Sambamba na hilo, Kamati inaisisitiza Serikali kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge walipokuwa wakichangia Azimio hilo.

2.2.27 Taarifa za Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vya Kibunge

Mheshimiwa Spika, uwakilishi wa Bunge katika Mabunge na Vyama mbalimbali vya Kibunge ni njia mojawapo ya kutekeleza Diplomasia ya Kibunge katika kuongeza ushirikiano mionganini mwa nchi mbalimbali, kuboresha uchambuzi wa taarifa za Serikali na kuwawakilisha vema Wananchi wa nchi Wanachama kwa kutetea maslahi yao Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa.

Mheshimiwa Spika, kupitia dhana ya Diplomasia ya Kibunge, Bunge lako ni mionganini mwa Mabunge mengi Duniani yanayoheshimu na kuthamini nafasi yake katika kuwezesha ushawishi mzuri wa mambo ambayo ni ajenda ulimwenguni vilevile kuchocha kasi ya kuridhia Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa na Tanzania pale ambapo Mikataba hiyo inaonekana kuwa na tija Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge ni dhahiri, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linapaswa kuendelea na utaratibu huu kwa maslahi ya Taifa na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachotolewa taarifa hii, Kamati ilipokea na kujadili taarifa za wawakilishi wetu kama ifuatavyo:-

i) ACP – EU

Mheshimiwa Spika, Bunge la pamoja la nchi za ACP (African Caribbean Pacific) na Umoja wa Ulaya (European Union) ni matokeo ya makubaliano ya Cotonue (The ACP-EU Partnership Agreement) ambapo nchi 78 za ACP isipokuwa Cuba ziliweka makubaliano ya kushirikiana na nchi 28 za Umoja wa Ulaya katika masuala ya Kisiasa, Kijamii, Kiuchumi, fedha, biashara na mazingira. Makubaliano hayo yalisainiwa tarehe 23 Juni, 2000 Jijini Cotonue Benin.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili taarifa ya wawakilishi hao, Kamati ilibaini kuwa ushiriki wa Bunge letu kwenye ACP/EU unapaswa kuendelezwa kwa kuzingatia kuwa jukwaa hili ni sehemu pekee ambayo sauti ya pamoja kwa nchi zinazoendelea inaweza kusikika.

Mheshimiwa Spika, naomba ifahamike kuwa Mkataba wa Ushirikiano kati ya Nchi za ACP na Umoja wa Ulaya unatarajiwa kumalizika mwezi Februari 2020. Kamati inaamini kuwa kumalizika kwa Mkataba huu ni fursa kwa nchi za ACP kuhakikisha kuwa makubaliano mapya yanalenga kunufaisha pande zote za ushirikiano na si Umoja wa Ulaya tu kama ilivyo sasa.

ii) SADC PF

Mheshimiwa Spika, Jukwaa hili ka Kibunge lilianzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, na kuwa moja ya Taasisi za SADC kwa mujibu wa kifungu cha 9 (2) cha Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo kusini mwa Afrika (SADC).

Mheshimiwa Spika, Jukwaa hili lilianzishwa kwa dhumuni la kupata sehemu ambayo Mabunge na Wabunge wa nchi Wananchama wanaweza kubadilishana uzoefu na mawazo chanya ili kuimarisha mshikamano wa nchi husika Kisiasa, Kijamii na Kiuchumi. Aidha, kwa siku za usoni, inategemewa Jukwaa hili kuwa Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika kama ilivyo kwa Kanda nyinginezo ambazo tayari zina Mabunge yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipofuutilia uwakilishi wa Bunge letu katika SADC PF ilibaini kuwa Bunge letu linadaiwa Randi 2,552,852/= ikiwa ni mchango wa Uanachama kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kamati inaona kuwa deni hili lisipolipwa mapema linaweza kuathiri taswria ya Bunge letu katika Jukwaa hilo.

iii) **Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola- CPA**

Mheshimiwa Spika, CPA ni mojawapo ya Vyama vya Kibunge vya muda mrefu. Chama hiki kilianzishwa Mwaka 1911 nchini Uingereza kwa ajili ya kuunganisha Mabunge katika nchi ambazo zilikuwa chini ya Himaya ya Uingereza. Lengo la Chama hiki, pamoja na mambo mengine, ni kuwasaidia Wanachama kujenga Mifumo ya Utawala wa Kidemokrasia na Utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ndio Makao Makuu ya Chama hiki kwa upande wa Afrika, na kwa mujibu wa Katiba ya CPA Tawi la Afrika, Mtendaji Mkuu wa Chama hiki kwa upande wa Afrika ni Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jambo hili limeiweka Tanzania, hususan Bunge lako Tukufu kuwa na nafasi ya kipekee katika CPA na inapaswa kutunzwa na kuheshimiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujadili taarifa zote za wawakilishi hao, Kamati ilibaini kuwa kutopatikana kwa fedha kwa ajili ya kushiriki Mikutano

kumeendelea kuwa changamoto iliyoathiri fursa ya Wawakilishi kushiriki ipasavyo katika masuala muhimu yaliyokuwa yanajadiliwa katika Mikutano hiyo.

2.3 Matokeo ya Semina zilizofanyika

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishiriki na kuongoza Semina tofauti Tatu katika kipindi cha Septemba, Oktoba na Novemba, 2017. Semina hizo zilihusu Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa; Dhana na utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau; na Uchambuzi wa Miswada ya Sheria na udhibiti wa Sheria Ndogo katika Bunge la Tanzania.

Katika Semina hizo, pamoja na mambo mengine, Wajumbe walijadili hatua na mbini za kuchambua Miswada ya Sheria; hatua za utungaji wa Sheria Ndogo na nafasi ya Bunge katika udhibiti wake; hatua za utayarishaji wa Mikataba ya Kimataifa; na aina za utekelezaji wa dhana na namna ya kutekeleza utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau.

Mheshimiwa Spika, katika Semina hizo, changamoto mbalimbali zilibainika kwenye baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

a) Diplomasia ya Kibunge na namna bora ya kusaini na kuridhia Mikataba ya Kimataifa

- i) Mikataba ya Kimataifa iliyosainiwa kuchukua muda mrefu kuridhiwa jambo ambalo linachelewesha Nchi/Wananchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye Mikataba hiyo;
- ii) Sheria za nchi kutoaanishwa na Mikataba au Itifaki za Kimataifa zilizoridhiwa jambo linalosababisha mkanganyiko kati ya Sheria ya Kimataifa (International Law) na Mfumo wa Sheria za Nchi; na
- iii) Wawakilishi wa Bunge kutokutana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kabla ya kuhudhuria Mikutano ya Vyama vyta Kibunge jambo ambalo linasababisha

wawakilishi hao kutokuwa na msimamo wa pamoja na Bunge katika masuala yanayoenda kujadiliwa katika mikutano hiyo.

b) Dhana na Utaratibu wa kusikiliza maoni ya Wadau

- i) Hisia kwamba maoni ya Wadau yanakusanywa kwa jambo ambalo uamuzi wake unajulikana na kwamba maoni yatakayotolewa hayawezi kuathiri uamuzi huo jambo ambalo linasababisha utaratibu huo kutothaminiwa na baadhi ya Wananchi; na
- ii) Tofauti ya kiuelewa mionganini mwa Wataalamu na Wananchi wengine (expert-citizen divide).

c) Udhhibitit wa Sheria Ndogo

- i) Upungufu wa Wataalam wa uandishi wa Sheria (Legislative Drafters) katika Serikali na vyombo vyake jambo ambalo linasababisha Sheria Ndogo nyingi kuwa na dosari. Wataalamu wanaotegemewa kuboresha maudhui ya Sheria Ndogo ni wale waliopo kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria ambao nao ni wachache ikilinganishwa na majukumu walijonayo; na
- ii) Serikali kuchelewa kuchapisha Sheria Ndogo zilizofanyiwa marekebisho jambo linalosababisha Sheria Ndogo zenye dosari kuendelea kutumika na hivyo kuleta athari kwa watumiaji.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha matokeo ya uchambuzi wa Kamati katika Sehemu ya Pili, naomba sasa kuwasilisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

a) Masuala ya Jumla

Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kunaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwenye Wizara zote zinazosimamiwa na Kamati hii.

b) Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

- i) Jeshi la Polisi limeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali za kibajeti zinazoathiri utendaji wa Jeshi hilo katika kusimamia usalama wa Raia na mali zao;
- ii) Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 ina mapungufu yanayochangia uwepo wa tatizo sugu la ajali za barabarani;
- iii) Ucheleweshwaji wa kutoa taarifa rasmi kwa Umma kuhusu hatua zilizofikiwa katika upelelezi wa matukio ya muda mrefu na yanayovuta hisia za Jamii kama vile matukio ya mauaji, kutekwa na kupotea kwa Viongozi na Wananchi mbalimbali kunasababisha Wananchi kutokuelewa hatua za upelelezi zilozofikiwa;
- iv) Kutokuwepo kwa utaratibu rasmi wa ulinzi kwa Wabunge katika makazi yao kunahatarisha usalama wao hasa kwa kuzingatia kuwa, baadhi ya majukumu yao katika kuisimamia Serikali yanagusa maslahi ya Watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;
- v) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa *Parole* na matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kunachangia kwa kiasi kikubwa msongamano wa wafungwa magerezani;

- vi) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa kunachangia msongamano wa wafungwa wa aina hiyo;
- vii) Kutokutolewa kwa fedha za miradi kwa Jeshi la Zimamoto kwa kipindi cha Miaka Miwili mfululizo kunaathiri utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na Mifumo na juhudzi za uokoaji na zimamoto;
- viii) Kutokuwa na suluhisho la kudumu kwa tatizo la Wakimbizi nchini kunaendelea kuhatarisha usalama katika maeneo wanayoishi na yale yanayowazunguuka; na
- ix) Madeni makubwa ya Wazabuni kwa Idara ya Uhamiaji yanasaababisha Idara hiyo kushindwa kupata na kutoa Hati za Kusafiria (Passports) kwa wakati.

c) Wizara ya Ulinzi na JKT

- i) Kukosekana kwa Sera ya Ulinzi wa Taifa nchini (National Defence Policy) kunaathiri ufanisi katika uratibu wa ulinzi wa Taifa;
- ii) Kukosekana kwa alama za mipaka ya nchi (beacons) kunachangia uvamizi wa shughuli za binadamu katika maeneo hayo jambo ambalo si zuri kwa ulinzi na usalama wa nchi;
- iii) Ubovu wa barabara za mipakani unasaababisha ugumu wa kufanya doria na kudhibiti mipaka ya nchi;
- iv) Madeni kwa mashirika yaliyo chini ya SUMA JKT yanaathiri shughuli za uzalishaji mali wa Shirika hilo;
- v) Wananchi kutolipwa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi kumeendelea kusababisha migogoro ya ardhi kati ya Wananchi na vikosi vya Jeshi hilo;
- vi) Muda wa miezi Mitatu kwa ajili ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria haukidhi katika kuwajengea moyo wa uzalendo vijana wala kuwaandaa kuwa Jeshi la akiba; na

- vii) Baadhi ya Wizara kutokutenga fedha kwa ajili ya mafunzo ya Maafisa waandamizi katika Chuo cha Ulinzi kunasababisha Maafisa hao kutohudhuria Kozi hizo muhimu za usalama na uongozi.

d) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

- i) APRM Tanzania kutokuwa na Fungu lake la Kibajeti kunaathiri utendaji wake kutokana na ufinyu wa bajeti;
- ii) Kutokutoa kipaumbele katika kushughulikia changamoto zinazokikabili Chuo cha Diplomasia kunahatarisha Chuo hicho kufutiwa Usajili wa NACTE;
- iii) Kukosekana kwa *National Convention Bureau* kunaikosesha nchi fursa ya kuvutia Mikutano na maonesho ya Kimataifa mengi zaidi kufanyika hapa nchini;
- iv) AICC kutokuwa na majengo yakutosha kwa ajili ya shughuli za Mikutano unakiondolea Kituo hicho ufanisi kwa kushindwa kushindana katika soko;
- v) Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi katika Balozi hizo;
- vi) Kutokarabati majengo ya Balozi zetu si tu kunashusha thamani ya majengo hayo yaliyonunuliwa kwa fedha nyingi, lakini pia kunaathiri taswira ya nchi yetu nje ya nchi;
- vii) Kukosekana kwa Sera ya Taifa kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki ni jambo la hatari katika mustakabali wa nchi;
- viii) Sera ya Mambo ya Nje ni ya muda mrefu na mchakato wa kuifanya marekebisho unachukua muda mrefu kukamilika;
- ix) Ucheleweshwaji wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa na Itifaki iliyosainiwa kunachelewesha nchi/Wananchi kunufaika na masuala muhimu yaliyo kwenye mikataba hiyo; na

- x) Kutooanisha Sheria za Nchi na Mikataba au Itifaki za Kimataifa zilizoridhiwa kunasababisha mkanganyiko kati ya Sheria za Kimataifa na Mfumo wa Sheria za nchi.

e) Wawakilishi wa Vyama vyta Kibunge

- i) Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Vyama mbalimbali vyta Kibunge kutoshiriki kikamilifu Mikutano ya Vyama hivyo kunaleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu ya Diplomasia ya Kibunge;
- ii) Wawakilishi wa Bunge kutokutana na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kabla ya kuhudhuria Mikutano ya Vyama vyta Kibunge kunaweza kusababisha wawakilishi hao kutokuwa na msimamo wa pamoja na Bunge katika masuala yanayoenda kujadiliwa katika mikutano hiyo.

3.2 Mapendeleko

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza maoni, naomba sasa kutoa mapendeleko ya Kamati kama ifuatavyo:-

3.2.1 Kutokutolewa kwa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

Kwa kuwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 hazikutolewa kwa ukamilifu, jambo ambalo lilikwamisha utekelezaji wake,

Na kwa kuwa kutokutekelezwa kwake kumesababisha hasara kutokana na madeni ya kimkataba na riba, na kuwalipa wasimamizi wa miradi hiyo bila kutekeleza majukumu yao ya msingi,

Kwa hiyo basi, Serikali itoe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge ili kufanikisha azma yake kwa miradi hiyo.

3.2.2Jeshi la Polisi kukabiliana na Uhalifu

Kwa kuwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuliwezesha Jeshi la Polisi kukabiliana na vitendo vya uhalifu ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya mafuta, magari, operesheni mbalimbali na vitendea kazi,

Na kwa kuwa ufinyu huo wa bajeti unaathiri utekelezaji wa majukumu yaliyokuwa yamepangwa kutekelezwa hususan operesheni mbalimbali za kuzuia uhalifu, upeletezi wa makosa mbalimbali ya jinai, operesheni za baharini na Maziwa Makuu,

Kwa hiyo basi, Serikali iongeze Bajeti ya Jeshi la Polisi na kutoa fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili Jeshi hilo liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Mikoa ambayo takwimu zinaonesha kiwango cha uhalifu kipo juu, ipewe kipaumbele.

3.2.3Hali ya ulinzi na usalama wa Raia na mali zao

Kwa kuwa matukio yanayohatarisha hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao yamekuwa yakijirudia na hivyo kujenga hofu mionganoni mwa Wananchi;

Na kwa kuwa, taarifa za hatua zilizofikiwa katika upeletezi wa matukio hayo zimekuwa hazitolewi mara kwa mara kwa Umma;

Kwa hiyo basi, Jeshi la Polisi liwe na utaratibu mahsuswa kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua zilizofikiwa katika upeletezi wa matukio ya muda mrefu ambayo yamevuta hisia za Jamii kama vile mauaji na kupotea kwa Wananchi mbalimbali.

3.2.4 Ulinzi na Usalama wa Wabunge

Kwa kuwa, hakuna Sheria wala Kanuni inayoelekeza Wabunge kupewa ulinzi katika makazi yao na hivyo kuliacha suala la ulinzi na usalama wa Wabunge kuwa jukumu la Mbunge mwenyewe;

Na kwa kuwa, kazi za Wabunge katika kuisimamia Serikali zinagusa maslahi ya Watu au makundi binafsi ambayo yanaweza kujenga chuki dhidi yao;

Kwa hiyo basi, Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ifanyiwe Marekebisho ili:-

- i) Kuweka sharti kwa Wabunge kupatiwa ulinzi hususan katika makazi yao wanapokuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kibunge Mjini Dodoma na katika maeneo yao ya uwakilishi; na
- ii) Kuweka utaratibu wa kutoa namba maalum za usajili wa magari ya Wabunge.

Aidha, Serikali iboreshe na kuimarisha ulinzi katika Maeneo ya Maegesho ya Magari Bungeni.

3.2.5 Msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani

Kwa kuwa tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu katika magereza nchini limeendelea kuwa sugu kutokana na:-

- i) Matumizi hafifu ya Sheria zinazoruhusu adhabu mbadala kwa wafungwa kama vile kifungo cha nje na huduma kwa Jamii;
- ii) Mahabusu kutokupelekwa Mahakamani kwa muda uliopangwa;
- iii) Kutokutumika ipasavyo kwa mpango wa Parole;
- iv) Kasi ndogo ya kusikiliza mashauri yanayohusu mauaji na dawa za kulevyta; na

- v) Kutokutekelezwa kwa adhabu iliyotolewa dhidi ya wafungwa waliohukumiwa kunyongwa;

Na kwa kuwa hali hiyo inaathiri afya za wafungwa na mahabusu vilevile kuiongozea Serikali gharama za kuwatunza;

Kwa hiyo basi, Serikali:-

- i) Itekeleze Sheria inayowataka wahalifu wenyewe makosa madogo kupewa adhabu mbadala kama vile vifungo vyatya nje na huduma kwa jamii;
- ii) Izingatie kuwapeleka Mahabusu mahakamani kwa tarehe walizopangiwa;
- iii) Itekeleze ipasavyo utaratibu wa *Parole*;
- iv) Ihakikishe kuwa Kamati za Kusukuma kesi zinakutana mara kwa mara ili kuwezesha hukumu za kesi kutolewa kwa wakati;
- v) Itolee maamuzi suala la wafungwa waliohukumwa adhabu ya kunyongwa hadi kufa.

3.2.6 Utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu nje ya nchi

Kwa kuwa utaratibu wa kutuma fedha kwenye Balozi zetu unataka fedha hizo zipitishwe katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,

Na kwa kuwa utaratibu huo umebainika kuwa na urasimu usio wa lazima na hivyo kuchelewesha kutuma fedha kwa mtiririko unaotakiwa,

Kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka fedha katika Balozi moja kwa moja bila kuitisha Wizarani kama ilivyo kwa Halmashauri zote nchini ambapo fedha hutumwa moja kwa moja bia kuitisha kwa Makatibu Tawala wa Mikoa husika.

3.2.7 Uchakavu wa majengo ya Balozi za Tanzania

Kwa kuwa majengo mengi ya Balozi zetu nje ya nchi ni chakavu sana,

Na kwa kuwa kutokarabati majengo hayo kumeendelea kuiongezea gharama Serikali kwani baadhi ya Balozi zinalazimika kukodi majengo mengine mbadala,

Kwa hiyo basi, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali itoe fedha za ukarabati wa majengo ya Balozi kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa kuanza na Balozi ambazo majengo yake yapo katika hali mbaya zaidi.

3.2.8 Uendeshaji wa Chuo cha Diplomasia

Kwa kuwa kwa takribani Miaka 36, Chuo cha Diplomasia kimekuwa kikiendeshwa na Serikali ya Tanzania pekee baada ya Serikali ya Msumbiji kujitoa katika kuchangia bajeti na kushiriki katika shughuli zote za uendeshaji,

Na kwa kuwa Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imefanya jitihada mbalimbali za kuwasiliana na Serikali ya Msumbiji ili ishiriki kikamilifu katika uendeshaji wa Chuo hicho bila mafanikio,

Kwa hiyo basi, Serikali iisitisize Tume ya Pamoja ya Ushirikiano yaani *Joint Permanent Commission* ambayo ndiyo yenyeye dhamana ya kushughulikia tofauti za makubaliano ya uundwaji wa Chuo hicho, kulishughulikia suala hilo kikamilifu kufikia Mwezi Mei, 2018 na hatimaye kuweka wazi kwa mujibu wa Sheria, kwamba Chuo hicho sasa kimilikiwe na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3.2.9 Uwakilishi katika Vyama vya Kibunge

Kwa kuwa Wawakilishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano katika Mabunge na Vyama mbalimbali vya Kibunge wameshindwa kushiriki kikamilifu Mikutano ya Mabunge na Vyama hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti;

Na kwa kuwa kutoshiriki vikao hivyo kunaweza kuleta picha isiyo nzuri mbele ya Mabunge mengine na Vyama vyá Kibunge kuwa Bunge lako Tukufu halithamini umuhimu wa Diplomasia ya Kibunge,

Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuipatia Ofisi ya Bunge fedha zote zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kuwawezesha Wajumbe wa Vyama vyá Kibunge kushiriki Mikutano husika kama ilivyopangwa kwa mujibu wa Ratiba.

3.2.10 Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki

Kwa kuwa tangu Mwaka 1999 Tanzania ilipojiunga na Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki hajjawahi kuwa na Sera maalum kuhusu Mtangamano wa Afrika Mashariki,

Na kwa kuwa kutokuwa na Sera hiyo kunaifanya Serikali kutekeleza masuala mbalimbali ya Jumuiya hiyo bila ya kuwa na mwongozo wa Kisera jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa Taifa;

Kwa hiyo basi, Serikali iongeze kasi ya maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Afrika Mashariki na Mkakati wa utekelezaji wake.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukurani

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa kipindi cha Januari, 2017 hadi Januari, 2018. Ni imani ya Kamati kuwa fursa hii inayotokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15), ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, itasaidia kuliwezesha Bunge lako Tukufu kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, (Mb), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, (Mb) na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga, (Mb), na watendaji wote wa Wizara hizo kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote ambacho Kamati imekuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe kwa kuratibu vema shughuli za Kamati kwa kipindi chote cha Mwaka mzima na hata kufanikisha kukamilika taarifa hii kwa wakati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza shughuli zilizotekelozwa, Uchambuzi wa matokeo ya utekelezaji wa shughuli za Kamati, Maoni na Mapendekezo sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa lipokee, lijadili na hatimaye kuikubali Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama pamoja na Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb

MWENYEKITI

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

09 Februari, 2018

TAARIFA ZILIZOPOKELEWA NA KUJADILIWA NA KAMATI**1. Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu:-**

- i. Hali ya Ushirikiano wa Kikanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Mtangamano wa Afrika Mashariki;
- ii. Utekelezaji wa majukumu ya Balozi za Tanzania katika Mashirika ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa (Multirateral Missions)
- iii. Utendaji wa Chuo cha Diplomasia, mafanikio na changamoto;
- iv. Utendaji wa *African Peer Review Mechanism* (APRM) Tanzania, mafanikio na changamoto;
- v. Utendaji wa kituo cha Kimataifa cha Arusha (Arusha International Conference Centre), mafanikio na changamoto; na
- vi. Utendaji wa kituo cha Kimataifa cha Julius Kambarage Nyerere (Nyerere International Conventional Centre), Mafaniko na Changamoto.

2. Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu:-

- i. Hali ya Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao;
- ii. Changamoto za kibajeti zinazolikabili Jeshi la Polisi katika kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao;
- iii. Utekelezaji wa Kazi za Jeshi la Polisi nchini; mafanikio na changamoto;

- iv. Utekelezaji wa Jeshi la Magereza ikiwemo Shirika la *Prisons Corporation Sole* (PCS); mafanikio na changamoto;
- v. Utekelezaji wa Kazi za Jeshi la Zimamoto; mafanikio na Changamoto;
- vi. Utekelezaji wa Kazi za Idara ya Uhamiaji; Mafanikio na Changamoto; na
- vii. Huduma kwa Wakimbizi nchini.

3. Taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu:-

- i. Utekelezaji wa kazi za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ikiwemo Shirika la SUMA JKT , Mafanikio na Changamoto;
- ii. Hali ya Mipaka ya Nchi;
- iii. Utendaji wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi, Mafanikio na Changamoto.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA CHAMA CHA MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA
(CPA TANZANIA) TAWI LA TANZANIA KWA KIPINDI CHA OKTOBA, 2017-JANUARI,
2018**

**KWA AJILI YA KUWASILISHWA KWENYE KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

**TAREHE 23 JANUARI, 2018
DODOMA**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu aliyenipa nafasi hii adhimu kuwasilisha taarifa hii muhimu ya utekelezaji wa majukumu ya Chama cha Mabunge ya Jumuia ya Madola tawi la Tanzania kwa kipindi cha Oktoba, 2017 hadi Januari 2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 7(2)(iv) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa Kamati yako kufahamu kwa kina kuhusu ushiriki wa Bunge la Tanzania katika vyama mbalimbali vya Kibunge vya Kimataifa na kwa sababu hii chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola tumepata nafasi hii muhimu ili wajumbe wa Kamati yako wapate uelewa wa kutosha kuhusu chama hiki, malengo yake, shughuli tunazozifanya na changamoto tulizonazo na namna bora ya kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa chama kwa faida ya Bunge la Tanzania na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema kwa ufupi Kamati yako ikafahamu historia ya chama hiki ili kujenga ufahamu mpana wa chama. Chama hiki kilianzishwa mnamo mwaka 1911 pale Uingereza kwa ajili ya kuunganisha Mabunge katika nchi ambazo zilikua chini ya himaya ya Uingereza. Tawi la kwanza la chama hiki kilianzishwa pale Uingereza. Nchi wanachama wa kwanza kabisa wa chama hiki zilijumuisha Australia, Canada, New Zealand, South Africa na Uingereza. Leo hii chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola kina wanachama zaidi ya 50 ulimwenguni kote kutoka Africa, Asia, Caribbean na nchi za Pasifikasi zilizokua chini ya Himaya ya Uingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekua na nafasi ya kipekee sana kwa upande wa chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola kwa upande wa Africa kwa sababu mara tu baada ya Zimbabwe kujitoa katika chama hiki mwaka 2003 Tanzania ilichukua jukumu la kuwa makao makuu ya Chama hiki kwa upande wa Afrika na kwa mujibu wa Katiba ya CPA Tawi la Afrika mtendaji Mkuu wa chama hiki kwa

upande wa Afrika ni Katibu wa Bunge la Tanzania ambaye anasaidiwa kwa karibu na Katibu Msaidizi wa Chama hiki ambaye anakua ni mtendaji mkuu wa Chama kwa upande wa Afrika. Kwa Muktadha huu mtendaji mkuu wa CPA Tawi la Afrika kwa sasa ni Katibu wa Bunge la Tanzania ndugu Stephen Kagaigai anayesaidiwa na Katibu Mkuu Msaidizi ndugu Demetrius Mgalmi.

2. MADHUMUNI YA CHAMA CHA MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa mujibu wa Katiba ya CPA,madhumuni makuu ya chama hiki ni kama ifuatavyo;

- i. Kuwasaidia wanachama kujenga mifumo ya utawala wa kidemokrasia na utawala wa Sheria (Rule of Law),
- ii. Kuujenga Umoja wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola duniani kote na kuhakikisha Umoja huu unazingatia Demokrasia na Utawala bora,
- iii. Kukuza maendeleo ya Kitaaluma ya wanachama na wafanyakazi wa Mabunge,
- iv. Kuupa nguvu umoja huu kuanzia ngazi ya tawi,kanda na katika ngazi ya Kimataifa kupitia Mawasiliano,
- v. Kutoa msaada wa utaalamu wa Kishauri kwa mabunge yanayotoka katika nchi changa na kujenga uwezo wao katika masuala mbalimbali,
- vii. Kukuza masuala ya usawa wa kijinsia ndani ya CPA na miongoni mwa wanachama kwa ujumla,
- viii. Kupigania na kutetea maslahi ya matawi madogo dogo yaliyo wanachama wa umoja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha ufanisi katika utendaji kazi wake, Chama cha Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola

kimegawanyika katika kanda kuu tisa zifuatazo; Afrika, Asia, Australia, Visiwa vya Uingereza na Mediterenia, Canada,Carribean, Americas and Atlantic (CAA), India, Pacific na Asia ya Kusini Mashariki (South East Asia).

3. CHAMA CHA JUMUIYA YA MADOLA TAWI LA TANZANIA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uongozi wa Tawi la Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya madola Tawi la Tanzania yaani Kamati ya Utendaji ya Tawi unaundwa na wanachama wafuatao ambao walichaguliwa na Wabunge katika Bunge hili la 11;

- i. Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mb, Mwenyekiti.
- ii. Mhe. Tundu Antifasi Lissu, Mb, Makamu Mwenyekiti
- iii. Mhe Maria Ndilla Kangoye, Mb, Mwakilishi wa Tawi CPA African Region Ex Com
- iv. Mhe. Amina Mollel, Mb, Mjumbe,
- v. Mhe. Dr. Sware Samesi, Mb, Mjumbe,
- vi. Mhe. Zainabu Vullu, Mb, Mjumbe,
- vii. Mhe. Mtumwa Khamis Mb, Mjumbe
- viii. Mhe Jitu Patel Soni, Mb, Mjumbe,
- ix. Mhe Japhet Hasunga, Mb, Mjumbe,
- x. Mhe Salum Rehani, Mb, Mjumbe,
- xi. Mhe. Juma Hamadi Omar, Mjumbe.

4.0 Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Taarifa hii fupi ni kuonyesha utekelezaji wa shughuli za chama kwa kipindi cha Novemba 2017 mpaka Januari 2018. Naomba sasa kwa heshima na taadhima nijielekeze katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kipindi hiki CPA Tawi la Tanzania lilishiriki katika mikutano miwili ya kimataifa na kiliandaa mpango kazi wa mwaka 2018 kama ifuatavyo.

4.1 MKUTANO WA 48 WA CHAMA CHA MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA KANDA YA AFRIKA

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majukumu makubwa ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola ni kukuza uhusiano kati ya Mabunge wanachama na mshikamano mionganini mwao. Katika kufikia lengo hili vyama mbalimbali vya CPA kutoka kanda mbalimbali huwa vinakutana kila mwaka kwa ajili ya kujadili na kuamua kuhusu masuala mbalimbali yanayowahusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CPA Tawi la Tanzania lilishiriki katika Mkutano wa 48 wa Chama cha Jumuiya ya Madola Tawi la Afrika ambao ulifanyika katika mji wa Oweri, Jimbo la Imo huko Nigeria kuanzia tarehe 20-26 Oktoba, 2017. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huu uliongozwa na Mhe. Naibu Spika, Dr. Tulia Ackson. Mjumbe mwingine aliyeshiriki Mkutano huu alikua Mhe. Amina Mollel, Mb pamoja na maafisa wa Ofisi binafsi ya Mheshimiwa Naibu Spika na afisa Bunge mmoja aliyeulewa na Katibu wa Bunge kama Katibu wa Msafara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe mkuu katika Mkutano huu ulikuwa "Agenda ya Afrika Mpaka kufikia Mwaka 2063, Maono na Mikakati Mikuu". Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huu ulishiriki katika vikao mbalimbali vya Chama cha Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Tawi la Afrika kwa lengo la kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za utekelezaji kutoka kwa vyama mbalimbali vilivyo katika kanda ya Afrika kama vile Chama cha Wanawake Wabunge wa Jumuiya ya Madola Kanda ya Africa (CWP), Chama cha Makatibu mezani (SOCCAT) na vyama vya Kikanda. Mkutano huu pia ulipokea taarifa ya utekelezaji kutoka Kamati kuu ya utendaji(EXCOM) Kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tawi la Tanzania lilipata heshima kubwa katika Mkutano huu baada ya Mheshimiwa Naibu Spika kuteuliwa kuwa

mjumbe wa Kamati Maalumu ya Mabadiliko ya Katiba ya Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Tanzania pia ilipata sifa kubwa sana kati ya nchi nyingi zilizohudhuria mukutano huu kutokana na ukuaji mzuri wa uchumi na utayari wake wa kuendelea kuchangia kiasi cha dola 45000USD kwa ajili ya uendelezaji wa Sekretariati ya Chama hiki kwa Kanda ya Afrika ambayo Ofisi yake ilipo Ofisi ndogo ya Bunge Dar es Salaam.

4.2 MKUTANO WA 63 WA CHAMA CHA MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA DUNIANI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe kutoka katika Mabunge wanachama hukutana mara moja kila mwaka katika Mkutano wa Mwaka wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Duniani kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa Shughuli za Chama.

Kwa mwaka 2017 Mkutano huu ulifanyika huko Dhaka, Bangladesh kuanzia tarehe 1-8, Novemba. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huu uliongozwa na Mhe. Naibu Spika Dr. Tulia Ackson. Wajumbe wengine wa Tanzania katika Mkutano huu walikua Mhe. Dr. Raphael Chegeni, Mhe.Zainabu Vullu, Mhe.Mariam Msabaha pamoja na maafisa kutoka Sekretariati ya Bunge. Dhumuni la Mkutano wa mwaka huu ilikuwa ni kujadili mambo mbalimbali hasa maeneo ya:-

- i) Mabadiliko ya Tabia ya Nchi (*Climate Change*);
- ii) Tatizo la Rushwa;
- iii) Ushiriki wa Wanawake kwenye Uongozi;
- iv) Ushiriki wa Vijana; na
- v) Mambo mbalimbali yanayotokea Duniani kwa sasa

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Mkutano huo jumla ya Semina nane (8) zilifanyika na jumla ya midahalo minne (4) ilifanyika ili kujadili mambo muhimu yanayozikumba nchi za Jumuiya ya Madola. Aidha, tofauti na miaka mingine mwaka huu waliongeza mdahalo wa vijana

ambapo vijana walishiriki kwenye mdahalo huo na kutoa mapendekezo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya ajenda kubwa za Mikutano Mkuu wa CPA wa Dhaka, Bangladesh ilikuwa ni kuchagua Mwenyekiti wa CPA Duniani. Katika uchaguzi huu kulikuwa na wagombea watatu; Mhe. Shirley M. Osborne, Mhe. Nikki Pattle na Mhe. Emilia Monjowa Lifaka. Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika kiliamua kumuunga mkono mgombea Emilia Monjowa Lifaka ambaye ni naibu Spika wa Bunge la Cameroon ambaye alishinda kwa kura 102 kati ya kura 192 na hivyo kutangazwa kuwa mshindi na Rais mteule wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola ulimwenguni kote.

4.3 UANDAAJI WA MPANGO KAZI KWA MWAKA 2018

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Novemba, 2017 mpaka 2018 chama kimekua katika maandalizi ya kuandaa mpango kazi ambao utatoa mwelekeo na vipaumbele vya shughuli za chama katika mwaka 2018. Moja kati ya vipaumbele vya chama katika mwaka 2018 ni kuona kwamba Tawi la Tanzania linashiriki kikamilifu katika shughuli za chama ndani na nje ya Afrika. Hii itawezekana kama Ofisi ya Bunge taongeza Bajeti ya Chama.

5. CHANGAMOTO

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili chama kiendelee vizuri ni lazima kiwe na ushiriki mzuri katika shughuli za Chama hasa Semina na Mikutano mbali mbali inayoandaliwa na Makao Makuu na Kanda na Matawi mali mbali. Tawi letu limekuwa likipokea mialiko lakini kutokana na uhaba wa rasilimali fedha hatukuweza kushirki mikutano ifuatayo:

i) CPA Post Election Seminar

Semina hii iliandaliwa na CPA Makao Makuu na ilipangwa kufanyika tarehe 2 – 3 Julai 2017. Kutokana na uhaba wa rasilimali fedha Semina hii ilihairishwa hadi hapo baadaye

ii) Safari za ziara za Mafunzo nje ya nchi zinazohusu CPA hazikufanyika kama ilivyo ada kutokana ha uhaba wa fedha

- iii) Pia chama kinahitaji kuwa na uwakilishi wa chama cha wabunge wanawake ndani ya Jumuiya ya Ulaya (Commonwealth Women Parliamentarians-CWP)
- iv) Kukosekana kwa afisa Dawati wa Chama katika Bunge la Tanzania kumepunguza ufanisi wa shughuli za chama katika Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kamati yako imesikia changamoto hizi naamini kabisa kwamba mamlaka inayouhsika itatoa msukumo unaostahili kwa Chama cha CPA Tawi la Bunge la Tanzania ili kuleta utekelezaji rahisi wa shughuli za chama katika Bunge la Tanzania.


5. HITIMISHO

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii muhimu mbele ya Kamati yako kwa ajili ya kuwasilisha taarifa fupi ya utekelezaji wa shughuli za chama kwa kipindi kilichotajwa. Napenda kuithibitishia Kamati yako kwamba chama kitaendelea kushirikiana na Kamati yako na kutoa taarifa za utekelezaji wa shughuli za chama kila kinapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha.

**Dr. Raphael Masunga Chegeni, MB.
Mwenyekiti wa CPA Tawi la Tanzania**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

TAARIFA YA WAWAKILISHI KWENYE JUMUIYA YA MABUNGE YA NCHI
ZA AFRIKA, KARIBIANI NA PASIFIKI (ACP) PAMOJA NA BUNGE LA
PAMOJA LA NCHI ZA ACP NA UMOJA WA ULAYA (ACP-EU JPA)

KWA KIPINDI CHA MWAKA 2017

KWA AJILI YA KUWASILISHWA KWENYE KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA

TAREHE 23 JANUARI, 2018

DODOMA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2)(a)(iii) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016 na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba kuwasilisha Taarifa ya shughuli za Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP) pamoja na Bunge la pamoja nchi za ACP na Umoja wa Ulaya (ACP-EU JPA) kwa mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutupa nafasi hii kwenye Kamati yako kama kanuni zinavyoelekeza. Huu ni utaratibu mzuri unaoweza kuongeza tija katika uwakilishi wetu na pia kwenye uanachama wetu katika Jumuiya hii ya kibunge ya ACP-EU.

Mweshimiwa Mwenyekiti, naomba kabla ya kuwasilisha taarifa hii niruhusu kwanza niwatambue Waheshimiwa Wabunge wanaoliwakilisha Bunge letu katika mikutano ya Jumuiya hii ambao ni:-

- i. Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb - Kiongozi wa Msafara
- ii. Mhe. Esther Matiko, Mb - Mjumbe
- iii. Mhe. Kemilembe Lwota, Mb -Mjumbe

2.0 MUUNDO NA UANACHAMA WA ACP-EU

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Makubaliano ya Georgetown ya mwaka 1975 na Makubaliano ya Cotonou ya mwaka 2000, mwanachama wa ACP-EU ni Bunge lolote ambalo nchi yake ni mwanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP) na Umoja wa Ulaya (EU) . Hivyo, muundo wa ACP-EU ni mjumuiko wa Maspika (*Presiding Officers*) na Wabunge waliochaguliwa kutoka Bunge mwanachama isipokuwa tu katika kuchagua wabunge hao mambo yafuatayo yatazingatiwa:

- (i) Kuhakikisha fursa sawa ya uwakilishi kwa wanawake na vyama vyaya siasa vyenye wabunge.
- (ii) Wanaochaguliwa kuwa Wawakilishi kwenye Jukwaa la Kibunge wasiwe na nafasi za uwaziri.
- (iii) Wawakilishi hao wataliwakilisha Bunge lao katika mikutano ya ACP na ACP-EU kwa kipindi cha miaka mitano.

2.1 Jumuiya ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP) uliundwa tarehe 6 Juni, 1975 kwa Makubaliano ya Georgetown. Umoja huo unajumuisha nchi 79 (nchi 48 za Afrika, nchi 16 za Karibiani na nchi 15 za Pasifikasi).

Malengo makuu ya Umoja huo ni yafuatayo:-

- (a) Kuwa na ushirikiano katika kuongeza kasi ya kuondoa umaskini katika nchi wanachama;
- (b) Kuratibu shughuli za ACP katika mfumo unaowezesha Umoja huo kuwa na sauti na msimamo wa pamoja katika masuala yanayohusu nchi zao kwenye mijadala na utekelezaji wa makubaliano baina yake na Umoja wa Ulaya;
- (c) Kuimarisha Umoja na mshikamano mionganini kwa nchi wanachama wa ACP pamoja na uelewa mionganini mwa watu wao;
- (d) Kuwa ni jukwaa la kuhimiza amani, utulivu, demokrasia na utawala bora duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kimsingi Umoja wa Nchi za ACP hutekeleza majukumu yake kupitia majukwaa yafuatayo:-

- (a) Wakuu wa Nchi Wanachama wa ACP (ACP Heads of State);
- (b) Baraza la Mawaziri kutoka Nchi Wanachama wa ACP (ACP Council of Ministers);
- (c) Jumuiya ya Mabunge ya Nchi za ACP (ACP Parliamentary Assembly) ambayo Bunge la Tanzania ni mwanachama.

2.2 Bunge la Pamoja la nchi za ACP na Umoja wa Ulaya (ACP-EU JOINT PARLIAMENTARY ASSEMBLY)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 23 Juni, 2000 kupitia Makubaliano ya Cotonou (ACP-EU Partnership Agreement), nchi za ACP isipokuwa Cuba

ziliweka saini makubaliano ya kushirikiana na nchi 28 za Umoja wa Ulaya (EU) katika masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, fedha, biashara na mazingira. Kupitia makubaliano hayo, likaundwa Bunge la Pamoja la nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi na Umoja wa Ulaya (*ACP-EU Joint Parliamentary Assembly*) ambalo kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Makubaliano ya Cotonou lina majukumu yafuatayo:-

- (a) Kuendeleza demokrasia kwa njia ya mazungumzo na mashauriano;
- (b) Kudumisha maelewano baina ya watu wa Mataifa ya Ulaya na watu wa nchi za ACP na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu masuala ya maendeleo;
- (c) Kujadili masuala yanayohusu maendeleo pamoja na mahusiano kati ya nchi za ACP na EU;
- (d) Kupitisha maazimio na kutoa mapendekezo kwa Baraza la Mawaziri la Pamoja la nchi za ACP na EU (*ACP-EU Joint Council of Ministers*) kwa lengo la kufikia malengo ya makubaliano; na
- (e) Kutetea maendeleo ya kitaasisi na kujengea uwezo mabunge ya nchi wanachama.

2.3 Taratibu za Uendeshaji wa Mikutano ya ACP-EU JPA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na taratibu za uendeshaji wa mikutano na vikao vya ACP-EU JPA zimeandaliwa na kufanyiwa marekebisho kupitia maazimio yaliyowekwa kwenye mikutano ya ACP-EU JPA. Aidha, Sera na taratibu hizo zinapatikana katika nyaraka zifuatazo:-

- (a) Makubaliano ya Cotonou yaliyofikiwa mwaka 2000 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2005 na 2010;
- (b) Kanuni za Uendeshaji (*ACP-EU JPA Rules of Procedure*) zilizotungwa tarehe 3 Aprili 2003 na kufanyiwa marekebisho tarehe 25 Novemba 2004, 23 Novemba 2006, 28 Juni 2007, 28 Novemba 2008, 18 Mei 2011, 29 Novemba 2012, 19 Jun1 2013 na 27 Novemba 2013.

2.5 Kamati za Bunge la Pamoja la ACP-EU

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na maelekezo ya ibara ya 25 ya Kanuni za Uendeshaji wa ACP-EU JPA Kamati tatu za kudumu zilianzishwa mwaka 2003 ambazo ni:-

- (a) Kamati ya Masuala ya Siasa;
- (b) Kamati ya Masuala ya Uchumi, Fedha na Biashara; na
- (c) Kamati ya Mambo ya Jamii na Mazingira

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kila mjambe wa Bunge la Pamoja anatakiwa kuwa mjambe wa Kamati moja kati hizo tatu. Kwa kuzingatia hilo, **Bunge la Tanzania ni mjambe wa Kamati ya Masuala ya Siasa ya ACP-EU JPA.**

Aidha, kama ilivyo kwenye Bunge la Pamoja la ACP-EU, Jumuiya ya Mabunge ya nchi za ACP pia huendesha shughuli zake kuitia Kamati tatu za aina hiyo hiyo ambazo hufanya kazi zake ndipo maazimio au masuala husika huwasilishwa kwenye Kamati za Pamoja za ACP-EU JPA. Lengo hasa ni kuhakikisha Bunge la pamoja (ACP-EU JPA) linajadili na kufikia maazimio yaliyopitiwa na kuridhiwa kwanza na ACP PA.

2.6 Utaratibu wa mikutano na vikao vya ACP-EU JPA

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wa ACP-EU JPA hukutana mara nne (4) kwa mwaka ikiwa mikutano miwili ni ya Bunge la Pamoja na mikutano mingine miwili ni kwa ajili ya uendeshaji wa vikao vya Kamati tatu za Kudumu za Bunge hilo.

Aidha, katika mikutano yote hiyo, Kamati ya Uongozi ya Bunge la Pamoja la nchi za ACP na EU (*Bureau of the ACP-EU Joint Parliamentary Assembly*) hukutana kwa ajili ya kuridhia shughuli za Kamati za Kudumu za Bunge hilo pamoja na kuridhia ratiba na rasimu za maazimio yatakayowasilishwa kwenye Bunge la Pamoja la ACP-EU kwa ajili ya kujadili na kufanya maamuzi.

3.0 MIKUTANO NA SHUGHULI MUHIMU ZILIZOFANYIKA KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JANUARI HADI DISEMBA, 2017

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Disemba, 2017 jumla ya mikutano minne (4) ilifanyika kama ifuatavyo:-

- (a) Vikao vya Kamati za ACP-EU JPA vilivyofanyika tarehe 20 na 24 Machi, 2017, Brussels Ubelgiji.
- (b) Mkutano wa 33 wa Bunge la Pamoja la ACP-EU uliofanyika kuanzia tarehe 17 hadi 21 Juni, 2017, St. Julian's, Malta.
- (c) Vikao vya Kamati za ACP-EU JPA vilivyofanyika tarehe 9 hadi 12 Oktoba, 2017, Brussels Ubelgiji.
- (d) Mkutano wa 34 wa Bunge la Pamoja la ACP-EU uliofanyika kuanzia tarehe 13 hadi 19 Desemba, 2017, Port-Au- Prince, Haiti (*Mkutano huu Tanzania haikushiriki*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mikutano hiyo shughuli muhimu zifuatazo zilifanyika:-

3.1 Kujadili na kupitisha Azimio kuhusu "Ufadhilli wa vyama vya siasa katika nchi za ACP na EU"(*Financing of political parties in ACP and EU countries*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe waliweza kupitia, kujadili na kupitisha Azimio kuhusu "**Ufadhilli wa Vyama vya Siasa katika nchi za ACP na EU**"(*Financing of political parties in ACP and EU countries*). Kwa kifupi, Azimio hilo limeainisha masuala yafuatayo kuhusu ufadhilli wa vyama vya siasa katika nchi za ACP na EU:-

- (a) Vyama vya siasa ni muhimu katika kukuza demokrasia lakini vimekuwa vikikabiliwa na upungufu wa vyanzo halali na vya uhakika vya fedha za kuendeshea shughuli zake na kugharamia uchaguzi. Katika nchi nyingi vyanzo vya fedha za vyama vya siasa ni michango ya wanachama, ushuru wa majengo na ofisi za kukodisha za vyama, faida kutoka kwenye

biasara za vyama, misaada kutoka kwa wananchi na wafanyabiashara, na ruzuku kutoka Serikalini.

Aidha, kwa sasa vyama vya siasa katika nchi za EU vinakabiliwa na upungufu wa wanachama wakati katika nchi nyingi za ACP kutohana na umaskini na upungufu wa rasilimali, wanachama hawana uwezo mkubwa wa kuchangia vyama.

- (b) Changamoto kubwa zilizopo sasa ni vyama vya siasa kutokuwa na vyanzo vya mapato vya kutosha kuviwezesha kushiriki kikamilifu katika kukuza demokrasia; Kutokuwepo kwa fursa sawa kati ya vyama tawala na vyama vya upinzani katika upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa vyama; Ufadhili haramu wa vyama vya siasa (*Illicit political party funding practices*); Uwezo wa makampuni makubwa ya kimataifa katika kushawishi kifedha au kuathiri matokeo ya uchaguzi; Uwakilishi mdogo wa wanawake katika siasa; na Uwezo mdogo wa serikali za nchi nyingi hususani za ACP katika kutoa ruzuku ya kutosha kwa vyama vya siasa.

Mhesimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizo, iliazimiwa yafuatayo yafanyike katika nchi wanachama ili kukabiliana na changamoto husika:-

- (i) Serikali za mataifa ya ACP na EU zihakikishe kunakuwa na mazingira mazuri ya kisiasa yatakayowezesha vyama vyote vya siasa kuwa na fursa nzuri ya kupata fedha za kutosha za kuendeshea shughuli za vyama na kugharamia uchaguzi.
- (ii) Vyama vya siasa kuwa na utaratibu wa kutangaza kwa umma vyanzo vyake vya mapato vya ndani na nje ili kudumisha uwazi na uwajibikaji katika upatikanaji na utumiaji wa fedha husika.
- (iii) Kuwepo kwa sheria na kanuni madhubuti za kudhibiti ufadhili haramu (*Illegal financing*) wa vyama vya siasa.

- (iv) Vyombo vya habari na asasi za kiraia zihakikishe zinafanya kazi kubwa ya kufichua vyama vya siasa vinavyofadhiliwa kwa njia au namna zinazokiuka sheria za nchi.
 - (v) Serikali za nchi za ACP na EU zihakikishe zinatenganisha vyanzo vya mapato ya Serikali na vyanzo vya mapato ya vyama tawala ili kukuza mazingira ya ushindani wa haki wa vyama vya siasa.
 - (vi) Nchi za ACP na EU ziandae miongozo ya ufadhilli wa Vyama vya Siasa katika mazingira ya uwazi kwa kuzingatia kuwa utawala bora kwa kiasi kikubwa huchangiwa na uwepo wa vyama vya siasa vyenye uwezo na ukomavu kisiasa na kiuchumi.
- 3.2 Kujadili na kupitisha Azimio kuhusu “Mchango wa michezo katika elimu na kuondoa umasikini” (***The role of sports as enabler for education and poverty eradication***)

Mhesimiwa Mwenyekiti, Wajumbe waliweza kupitia, kujadili na kupitisha Azimio kuhusu “Mchango wa michezo katika elimu na kuondoa umasikini” (*The role of sports as enabler for education and poverty eradication*). Aidha, lengo la kutaka kupitisha kwa pamoja (ACP na EU) Azimio hilo ilikuwa ni kushirikiana katika kuweka na kusimamia sera na mikakati ya kukuza sekta ya michezo katika nchi za ACP kama ilivyo kwenye Nchi za Ulaya ili sekta hiyo iweze kuchangia katika kukuza elimu na kukabiliana na umaskini kwa kutoa fursa za ajira, kipato na kuwajenga wananchi kiafya.

Mhesimiwa Mwenyekiti, Kupitia Azimio hili, Wajumbe walisisitiza kuwa changamoto zilizopo kwenye kukuza sekta ya michezo ni ukosefu wa fedha, utashi wa kisiasa katika kukuza sekta husika na ukosefu wa miundombinu ya michezo. Hivyo, wajumbe walisisitiza umuhimu wa Serikali za nchi za ACP kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukuza sekta hiyo, makampuni makubwa ya kimataifa yaliyowekeza kwenye nchi husika kusaidia katika kukuza sekta ya michezo, na EU ishirikiane na nchi za ACP katika kuandaa sera na

miongozo ya kuboresha na kukuza sekta ya michezo na kusimamia haki za wanamichezo kutoka nchi za ACP.

- 3.3 Kujadili na Kupitisha Azimio kuhusu "Changamoto na faida za Uchumi wa Bahari kwa nchi za ACP" (**Blue Economy; opportunities and challenges for ACP states**)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupitia Azimio hilo, Wajumbe walikubaliana kwamba Uchumi wa Bahari una uwezo wa kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye ukuaji wa uchumi na kuleta maendeleo katika nchi za ACP kupitia shughuli za biashara na utalii. Pia, ilionekana kuna hatari ya Nchi za ACP kukabiliwa na changamoto mbalimbali kama uvuvi haramu, uharibifu wa mazingira na matatizo ya kiusalama. Hivyo, Bunge la Pamoja la ACP-EU lilisitiza umuhimu wa kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari katika nchi za ACP, ili kuongeza uwezo wa nchi hizo kukabiliana na changamoto tajwa. Aidha, Nchi za EU na nchi za ACP zilikubaliana kutafuta namna bora ya kushirikiana ili uchumi wa bahari uweze kunufaisha nchi hizo.

- 3.4 Kujadili na kupitisha Azimio kuhusu "Kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za msingi, hususan madawa kwa ajili ya kupambana na magonjwa ya kuambukiza" (**Improving access to basic health systems, notably to medicines in the fight against infectious diseases**)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kupitia Azimio hilo, Wajumbe walikubaliana kwamba nchi nyingi za ACP zinakabiliwa na changamoto kubwa katika kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na magonjwa ya mlipuko kutokana na upatikanaji mgumu wa huduma za afya za msingi. Kati ya mambo yanayosababisha watu kukosa huduma hizo ni kutofautiana kati ya mahitaji halisi ya huduma za afya na jinsi soko la huduma hizo linavyoendeshwa, pamoja na huduma za afya kutopewa kipaumbele kinachostahili katika Bajeti za Serikali. Hivyo, Azimio hilo limesitiza umuhimu wa nchi za ACP kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za afya, kuweka utaratibu wa kiufanisi katika

kufuatilia na kudhibiti bei za madawa, pamoja na ushirikiano wa sera za maendeleo katika masuala ya kisheria na maamuzi yanayohusu sekta ya afya.

3.5 **Kujadili mada kuhusu athari za biashara haramu ya vifaa vya kilimo, mbegu na bidhaa nyingine za kilimo**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walipata fursa ya kujadili kwa kifupi mada juu ya Athari za biashara haramu ya vifaa vya kilimo, mbegu na bidhaa nyingine za kilimo kwenye uchumi wa nchi za ACP (*the impact of illegal trade in phytosanitary products seeds and other agriculture inputs on ACP countries*) kwa ufupi, wajumbe walikubaliana kuwa biashara hii ina athari kubwa kwa binadamu na hivyo walikubaliana kuwa ni muhimu nchi wanachama kutunga sheria kali ili kukomesha biashara hii.

3.6 **Kujadili hali ya kisiasa katika nchi ya Burundi**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mgogoro wa kisiasa nchini Burundi uliotokana na Rais wa nchi hiyo kugombea muhula wa tatu wa urais, Umoja wa Ulaya (EU) ulichukua hatua za kuiwekea vikwazo nchi ya Burundi ikiwa ni pamoja na kusimamisha misaada kwa Serikali ya Burundi. Umoja wa Ulaya ulidai kuwa hii ni kutokana na kutomalizwa mgogoro wa kisiasa nchini humo ilisababisha vifo vya zaidi ya watu 400 na kuwalazimisha watu zaidi ya 240,000 kukimbilia nchi za jirani.

Hivyo basi, kutokana na vikwazo hivyo, Mjumbe kutoka Burundi alieleza kuwa wananchi wao wanapata matatizo kutokana na vikwazo vilivyowekwa na Umoja wa Ulaya, hivyo aliomba nchi za ACP kuendelea kuwapatia ushirikiano ili vikwazo viondolewe.

Aidha, wajumbe walizisihi nchi za ACP kufanya mazungumzo na EU kwa lengo la kuisaidia Burundi kurudisha mahusiano yake na umoja huo ikizingatiwa kuwa Burundi bado inahitaji msaada wa kifedha na kiulinzi ili iweze kutoa misaada na huduma za msingi kwa jamii zinazoathirika na mgogoro wa kisiasa nchini humo.

3.7 Kujadili hali ya kisiasa katika nchi ya Kenya

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mkuu wa Oktoba, 2017 kilikuwa ni kipindi ambacho matokeo ya Uchaguzi wa Rais wa Kenya yalikuwa yamefutwa na Mahakama na Wakenya walikuwa wanaelekea kwenye uchaguzi wa marudio uliofanyika 26 Oktoba 2017. Hivyo, Mjumbe kutoka Kenya alieleza kuwa nchi yao baada ya kufanya uchaguzi wa awali, viongozi wa upinzani walienda Mahakamani kupinga matokeo na Mahakama ilibatilisha uchaguzi wa Urais. Alieleza kuwa nchi yao kwa miaka mingi imefuata demokrasia na hivyo wangefanya uchaguzi mwingine kwa kuzingatia misingi hiyo ya demokrasia waliyojiwekea. Hivyo, aliomba nchi za ACP kuendelea kuwapatia ushirikiano na ikibidi watume waangalizi wa uchaguzi nchini Kenya. Aidha, uchaguzi huo ulirudiwa na ulimalizika kwa amani.

3.8 Kujadili hali ya kisiasa katika nchi ya Mali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mjumbe kutoka Mali alielezea kuwa nchi yao imekumbwa na janga la magaidi ambao wamesababisha vifo vyta watu wengi na uharibifu. Hivyo, aliomba nchi za ACP kuendelea kuwasaidia katika jitihada zao za kupambana na ugaidi nchini mwao.

Aidha, alielezea kuwa Bunge lao limepitisha Sheria itakayowawezesha kufanya marekebisho Katiba ya nchi hiyo ili kuondoa mapungufu yaliyopo na alisisitiza kuwa Katiba hiyo ikifanyiwa marekebisho haitaondoa ukomo wa muda wa Urais kama watu wengi wanavyopotosha. Hata hivyo, kutokana na malalamiko mengi yaliyojitokeza Rais wa Mali aliamua kuhairisha zoezi la kura ya maoni iliyokuwa imepangwa kufanyika Julai 9, 2017.

3.9 Kujadili hali ya kisiasa katika nchi ya DRC CONGO

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mjumbe kutoka DRC alieleza kuwa kwa sasa nchi yao imepata mafanikio katika kutatua mzozo wa kisiasa uliokuwa unawakabili baada ya kuunda Serikali yenye kushirikisha

vyama vya upinzani. Hivyo aliomba ACP kuwapatia ushirikiano ili waweze kufanya uchaguzi.

3.10 **Mjadala kuhusu Visiwa vya Karibiani**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Karibiani zimewekwa kwenye kundi la nchi za uchumi wa kati, wakati huo huo zinakumbana na majanga mbali mbali mfano matetemeko ya ardhi, mafuriko na majanga mengine. Hivyo kwa kuziweka nchi za Karibiani kwenye kundi la nchi za uchumi wa kati ni kuzinyima fursa ya kupata misaada ya fedha kutoka Benki ya Dunia. Kutokana na hali hiyo, Mjumbe kutoka Karibiani aliwasihi Wajumbe kuwasaidia ili na wao waweze kupata misaada kukabiliana na majanga yanayowakumba mara kwa mara.

3.11 **Kumalizika kwa Mkataba wa Cotonou (CPA)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 9 Oktoba, 2017 kilifanyika kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Uongozi ya ACP, Mabalozi kutoka nchi za ACP na Wajumbe wa Mkutano wa ACP. Wajumbe walijadili kuhusu aina ya ushirikiano mpya wa ACP na Umoja wa Ulaya (EU) baada ya kuisha kwa mkataba wa Cotonou mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kuwa Mkataba wa Ushirikiano kati ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP) na Umoja wa Ulaya (EU) uliosainiwa mjini Cotonou, Benin tarehe 23 Juni 2000 (*Cotonou Partnership Agreement - CPA*) unatarajiwa kumalizika mwezi Februari 2020. Mazungumzo kati ya nchi za ACP na Mataifa ya EU yenye lengo la kutathimini vipengele na masharti ya kuendesha ushirikiano mpya yanatakiwa kuanza kabla ya mwenzi Agosti 2018.

Kumalizika kwa Mkataba huo unaohusisha nchi 106 (Nchi 78 za ACP na 28 za EU) zenye jumla ya watu bilioni 1.5 kunatoa fursa kwa nchi husika kuboresha ushirikiano na mahusiano kati ya pande hizo mbili kwa kuelekeza nguvu kwenye kufanikisha maslahi, malengo na majukumu ya pamoja(*Partnership on common interests, objectives and shared responsibilities*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walifahamishwa kuwa, mwaka 2016 Wakuu wa nchi mbalimbali za ACP katika vikao vyao walifanya maamuzi kuwa ACP lazima ifanyiwe mabadiliko baada ya kumalizika kwa Makubaliano ya Cotonou mwaka 2020 ili iweze kuwa na manufaa (*fit for purpose*) na kuandaa malengo, maeneo ya vipaumbele na msimamo wa pamoja wa nchi za ACP utakaotumika kwenye mazungumzo na EU. Hivyo basi, baada ya uamuzi huo ACP imekuwa inajaribu kutafuta njia za kuifanya iwe ni Taasisi yenye umuhimu duniani.

Katika kikao hicho cha Kamati ya Uongozi ya Mabalozi kutoka nchi za ACP na Kamati ya Uongozi ya ACP na Wajumbe, washiriki walipata fursa ya kujadili ili kuona aina na muundo wa mkataba mpya utakaofaa baada ya Mkataba wa sasa wa Cotonou kumalizika mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe walijadili kwa kina na kukubaliana kuwa utekelezaji wa Mkataba wa Cotonou na kati ya Mataifa ya EU na nchi za ACP haujatumika ipasavyo katika kuleta matokeo chanya kwenye nyanja za kimataifa. Katika majadiliano hayo wajumbe wengi walionyesha masikitiko yao kwa kuwa ushirikiano huo umeshindwa kwa kiasi kikubwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa hapo awali. Hii ni kwa kuwa kwa kiasi kikubwa ushirikiano huu umeonekana kuunufaisha zaidi Umoja wa Ulaya kuliko nchi za ACP.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wajumbe wengi walilalamikia ukosefu wa usawa baina ya Umoja wa Ulaya na nchi za ACP kwenye masuala mbalimbali hasa kwenye masuala ya uchumi na biashara. Kutokana na sababu hiyo, Wajumbe walishauri kabla makubaliano mapya hayajafikiwa nchi za ACP zikubaliane na ziwe na msimamo mmoja kwenye masuala yote ya msingi. Hii ni kwa kuwa tayari nchi nydingi za Afrika zina ushirikiano na China na zinahitaji fursa za kibiashara na siyo misaada kama ilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano makubwa katika kikao hicho, Wajumbe walipendekeza nchi za ACP zisiharakishe

kuingia kwenye makubaliano mapya ya kushirikiana na EU bila kufanya tathmini ya maeneo na masuala ambayo zingependa kushirikiana na EU kwa faida ya nchi husika. Aidha, Wajumbe walishauri mapendelekezo ya EU yafanyiwe tathmini na uchambuzi wa kina katika ngazi ya kitaifa na kisha kikanda kabla ya kuingia makubaliano yoyote mapya.

4.0 CHANGAMOTO

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Jumuiya ya Mabunge ya nchi za Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP) pamoja na Bunge la pamoja la nchi za ACP na EU, lakini bado kuna changamoto zinazolikabili Bunge hili kama ifuatavyo:-

- (a) Upungufu wa fedha za kuendesha shughuli za Bunge la nchi za ACP. Kwa miaka ya hivi karibuni Sekretarieti ya ACP imeshindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake kwa kukosa fedha za kutosha hii ni kwa sababu upatikanaji wa fedha za uendeshaji umekuwa ni changamoto.
- (b) Ukosefu wa uaminifu kati ya Nchi za Jumuiya ya Mabunge ya Ulaya (EU Parliament) na Jumuiya ya Nchi za Umoja wa Afrika, Karibiani na Pasifikasi (ACP). Nchi za ACP zimekuwa zikilalamika kuwa ushirikiano huu umeegemea upande mmoja ambapo EU mara nyingi imeshindwa kuheshimu maamuzi na maazimio yanayopitishwa na nchi za ACP.

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni ya wawakilishi wa Bunge la Tanzania katika mikutano ya ACP-EU ili Kamati yako iweze kuyatafutia suluhisho:- Maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

- (a) Kwa kuwa katika Mikutano hii kunajitokeza maswali mbalimbali kuhusiana na hali ya kisiasa na kiuchumi kitaifa, Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla, ni vizuri Serikali ikawa inatoa msimamo wa masuala hayo kwa ajili ya ujumbe unaokuwa unawakilisha nchi ili

kuepuka wawakilishi kutoa msimamo unaoweza kupingana na msimamo wa Serikali.

- (b) Jumuiya ya Mabunge ya nchi za ACP hutekeleza shughuli zake na kuwasiliana na Mabunge ya nchi wanachama kupitia Balozi za nchi hizo zilizopo Brussels Ubeltgiji. Hivyo, Bunge la Tanzania hupata taarifa za shughuli za ACP-EU kupitia ubalozi wetu uliopo Brussels, Ubeltgiji lakini kwa kipindi kirefu ubalozi wetu umekuwa ukikabiliwa na upungufu wa fedha ambao wakati mwingine husababisha kushindwa kutuma uwakilishi hususan kwenye mikutano inayofanyika nje ya Ubeltgiji. Hivyo, Kamati yako inaombwa kusimamia kwa karibu Bajeti ya Balozi zetu hususan Ubalozi wetu uliopo Brussels Ubeltgiji ili uwe na fedha za kushiriki kikamilifu katika shughuli za ACP-EU kwa manufaa ya Taifa.

6.0 SHUKRANI

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati yako kwa kuona umuhimu wa Taarifa hii kuwasilishwa kwenye Kamati na kwa kutusikiliza kwa umakini. Ombi letu kwenu ni kujadili vizuri Taarifa hii ili muweze kutushauri ipasavyo kuhusu masuala mbalimbali kama wawakilishi wenu kwenye mikutano na vikao vya ACP-EU, kuyafahamu mambo mbalimbali yanayoamuliwa na kuazimiwa katika mikutano hiyo, na kuhakikisha mambo ya msingi katika Taarifa hii yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Tunapenda pia kutoa shukrani kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa kwetu. Shukrani pia ziende kwa Ubalozi wa Tanzania nchini Ubeltgiji kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwetu wakati tukihudhuria Mikutano hiyo Brussels, Ubeltgiji.

Mwisho napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake unaotusaidia kuwa wawakilishi wazuri katika mikutano hiyo na Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuratibu vizuri safari zetu tunapoenda kushiriki kwenye shughuli za ACP-EU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha Taarifa hii kwenu ili muweze kuendelea na hatua zinazofuata.

.....

Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb
Naibu Spika wa Bunge

23 Januari, 2018

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA JUKWAA LA KIBUNGE LA NCHI
WANACHAMA WA JUMUIYA YA MAENDELEO YA KUSINI MWA
AFRIKA**

(SADC-PF) KWA KIPINDI CHA NOVEMBA, 2017 – JANUARI, 2018

**KWA AJILI YA KUWASILISHWA KWENYE KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

TAREHE 22 JANUARI, 2018

DODOMA

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wawakilishi kwenye Jukwaa la Mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC- PF) naomba kuwasilisha maelezo mafupi kuhusu Jukwaa hili la Kibunge mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, kwa mujibu wa Kifungu cha 7(2) (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kutoa shukurani zetu za dhati kwa kupangwa kwenye ratiba ya kikao hiki ili tuwasilishe taarifa yetu kwa Kamati hii kama kanuni zinavyohitaji. Ni utaratibu mzuri unaoweza kuongeza tija katika uwakilishi wetu na pia kwa uanachama wetu katika Jukwaa la Jumuiya hii na pia katika Jumuiya ya SADC kwa ujumla. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa ufupi kuelezea historia ya Jukwaa la Kibunge la nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC-PF).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jukwaa hili lilianzishwa mwaka 1997 Jijini Blantyre, Malawi kufuatia mkutano wa Wakuu wa nchi wanachama kukubali na kuitisha uwepo wa Jukwaa hilo (SADC PF) kama moja ya Taasisi za SADC kwa mujibu wa kifungu cha 9(2)¹ cha Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Madhumuni makubwa ya kuanzishwa kwa Jukwaa hili la kibunge ni kupata sehemu ambayo Mabunge na Wabunge kwa ujumla wa nchi wanachama wanaweza kubadilishana uzoefu na mawazo chanya ili kuimarisha mshikamano wa nchi husika kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Shabaha ya kuanzishwa kwa Jukwaa hilo kama ilivyodhihiri katika Mkutano wa Blantyre ni hatimaye kuwa na Bunge la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC-PARLIAMENT*) kama ilivyo kwa kanda nyinezo ambazo tayari zina Mabunge yao. Mfano wa Mabunge hayo ya Kanda ni Bunge la Afrika (PAP) na Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

Kwa sasa nchi wanachama wa Jukwaa hili la Kibunge ni 14 ambazo ni:

- Afrika ya Kusini, Angola, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Swaziland, Tanzania, Zambia na Zimbabwe na Makao Makuu ya Jukwaa hili Kibunge yapo Windhoek, Namibia.

Madhumuni ya kuanzishwa kwa Jukwaa la SADC – PF ni:-

- (i) Kushawishi utekelezaji bora wa sera na mipango ya SADC ikiwa ni pamoja na itifaki na mambo mengine ya kisheria.
- (ii) Kushawishi misingi ya Haki za Binadamu, usawa wa Jinsia, na Demokrasia katika kanda ya SADC.

- (iii) Kuhakikisha uwepo wa amani, usalama na demokrasia kwa nchi wanachama.
- (iv) Kushawishi dhana nzima ya maisha bora ya sasa na yajayo kwa watu wa kanda hii ili hatimaye kwa pamoja waweze kujitegemea na kuwa na tija katika uchumi.
- (v) Kuratibu mawasiliano na Wabunge/Mabunge mengineyo ikiwa ni pamoja na asasi za Kitaifa na Kimataifa.
- (vi) Kutoa ushawishi kwa vyama visivyokuwa vya kiserikali, asasi na jamii za kisomi kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za SADC.
- (vii) Kuwepo kwa Jukwaa kwa ajili ya majadiliano kwa mambo yanayogusa hisia za nchi wanachama.
- (viii) Kuhakikisha uwepo wa utawala bora, uwazi na uwajibikaji katika kanda hii ya SADC na pia katika taasisi za SADC.
- (ix) Kuratibu uridhiwaji na utekelezwaji wa sera na sheria kwa nchi wanachama.
- (x) Kushawishi na kuwaelimisha wananchi wa nchi wanachama wa SADC kujua dhamira na madhumuni ya SADC.
- (xi) Hatimaye Jukwaa hili kuwa Bunge la Kanda ya SADC.

2. UWAKILISHI

Kifungu cha 7 cha Katiba ya SADC PF kinaelekeza kuwa uanachama na muundo wa Jukwaa hili la Kibunge utakuwa na wawakilishi watano watakaochaguliwa na Bunge la Nchi Mwanachama. Kifungu hicho kinaelekeza kuwa katika mchakato wa kuwapata wawakilishi hawa kila Bunge la Taifa litahakikisha kuwa usawa wa kijinsia na uwakilishi wa vyama vyta siasa Bungeni unazingatiwa. Aidha, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wanawake (TWPG) anakuwa mjumbe kwa nafasi yake.

Mwakilishi kwenye Jukwaa hili la Kibunge atatumikia kuanzia tarehe aliyochanguliwa mpaka atakapokoma kuwa Mbunge au pale atakapoteuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri.

3. MUUNDO NA UANACHAMA WA SADC PF

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba ya SADC- PF, mwanachama wa SADC-PF ni Bunge lolote ambalo nchi yake ni mwanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika yaani SADC. Hivyo, muundo wa SADC PF ni msumuiko wa Maspika (*Presiding Officers*) na Wabunge watano (5) waliochanguliwa kutoka kila Bunge la nchi mwanachama isipokuwa tu katika kuchagua Wabunge hao mambo yafuatayo yazingatiwe:

- (i) Kuhakikisha fursa sawa ya uwakilishi kwa wanawake na vyama vyta siasa vyenye Wabunge.

- (ii) Katika nafasi hizo Tano (5) awepo Mwenyekiti wa chama cha Wabunge wanawake (*Women Parliamentarians Group*) ambaye ataingia kwa nafasi yake.
- (iii) Wanaochaguliwa kuwa Wawakilishi kwenye Jukwaa la Kibunge wasiwe na nafasi za Uwaziri.
- (iv) Wawakilishi hao wataliwakilisha Bunge lao katika SADC PF kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya uhai wa Bunge.

SADC PF ina vyombo vinne vyenye majukumu mbalimbali ambavyo ni:-

(i) **Mkutano Mkuu wa Kibunge (*Plenary Assembly*)**

Chombo hiki kinajumuisha Maspika na Wabunge wawakilishi wa SADC PF waliochaguliwa toka Mabunge wanachama. Pamoja na majukumu mengine chombo hiki kazi yake kubwa ni kutunga sera pamoja na kutoa maamuzi kuhusu jambo lolote lililokubaliwa na wanachama.

(ii) **Kamati ya Utendaji (*Executive Committee*)**

Chombo hiki kinajumuisha Maspika na Wabunge (Ordinary Member) ambao huteuliwa na Spika kutoka mionganini mwa wawakilishi kwa mchanganuo ufuatao; Maspika saba (7) na Wabunge (Ordinary Member) saba. Wajumbe wa Kamati hii hudumu kwa kipindi cha miaka miwili (2).

Kazi kubwa ya Kamati ya Utendaji ni kusimamia maslahi ya wawakilishi wa SADC PF, kutoa mwongozo kwa Watumishi wa Sekretarieti ya SADC PF na kuhakikisha kuwa maamuzi yote yaliyofikiwa na Mkutano Mkuu yanatekelezwa.

(iii) Ofisi ya Katibu Mkuu (*Office of the Secretary General*)

Katibu Mkuu ambaye huidhinishwa na Mkutano Mkuu baada ya kupata mapendekezo toka Kamati ya Utendaji. Huidhinishwa kila baada ya miaka mitano (5). Jukumu lake kubwa ni kuratibu shughuli zote za SADC-PF na kusimamia kazi za siku hadi siku za Jukwaa hili la Kibunge.

(iv) Kamati za Kudumu za SADC PF (*Standing Committees*)

Kwa mujibu wa Katiba ya SADC PF Mkutano Mkuu huunda Kamati za kudumu ili kurahisisha utendaji wa shughuli zake. Kamati hizo ni kama ifuatavyo;

- 1. Gender Equality, Women Advancement and Youth Development Committee*
- 2. Human and Social Development and Special Programs Committee*
- 3. Trade, Industry, Development and Integration Committee*

4. Food, Agriculture, Natural Resources and Infrastructure Committee

5. Democratization, Governance and Human Rights committee

Aidha, pamoja na kamati hizo kuna Umoja wa Kikanda wa Wabunge wanawake wa SADC (Regional Women Caucus).

4. WAJUMBE WAWAKILISHI WA KWENYE SADC- PF

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wajumbe wanaowakilisha Bunge letu la Tanzania katika SADC-PF pamoja na Kamati zao ni hawa wafuatao:-

- (i) **Mhe. Job Y. Ndugai, Mb**, Spika,
- (ii) **Mhe. Margaret S. Sitta, Mb**, Mjumbe, wa Kamati ya *Gender Equality, Women Advancement and Youth Development Committee*
pia huwakilisha kwenye *Regional Women's Parliamentary Caucus (RWPC)* ya SADC-PF
- (iii) **Mhe. Selemani J. Zedi, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Trade, Industry, Development and Integration Committee*, pia mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya SADC PF
- (iv) **Mhe. Ally A. Saleh, Mb**, Mjumbe wa Kamati ya *Democratization, Governance and Human Rights committee*

- (v) **Esther M. Mmasi, Mb,** Mjumbe wa Kamati ya *Food, Agriculture, Natural Resources and Infrastructure Committee*
- (vi) **Mhe. Jamal K. Ali, Mb,** Mjumbe wa Kamati ya – *Human and Social Development and Special Programs Committee*

5. SHUGHULI AMBAZO ZIMEFANYIKA KWA KIPINDI CHA NOVEMBA, 2017 – JANUARI, 2018.

Jukwaa hili la Kibunge hukutana mara mbili (2) kwa mwaka kwa mikutano yake ya Kibunge, pamoja na Mikutano hiyo, vikao vyatya kamati navyo hukutana mara mbili kwa mwaka. Mikutano ya Kibunge hufanyika kwa mzunguko kutoka mionganini mwa nchi wanachama kwa kadiri wanavyojitolea kuwa mwenyeji wa mikutano hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ratiba hiyo Kamati ya Utendaji nayo hukutano mara mbili (2) kwa mwaka. Aidha, Bunge huweza kushiriki shughuli mbalimbali ambazo husimamiwa na Jukwaa hili la Kibunge nje ya mikutano yake ambayo ipo kwa mujibu wa Katiba kwa kadiri fursa zinapopatikana.

Kwa kipindi cha kuanzia Oktoba, 2017 hadi Novemba, 2017 Bunge kuitia Wawakilishi wake walishiriki kwenye vikao vyatya Kamati na Mkutano Mkuu wa Kibunge wa 42 wa Jukwaa hili. Pamoja na mikutano hiyo Bunge lilishiriki katika semina na warsha mbalimbali zilizoandalisha na Jukwaa hilo.

5.1. Ushiriki wa Wajumbe kutoka Tanzania katika Mkutano Mkuu wa 42

Tanzania iliwakilishwa na Wajumbe 6 wakiongozwa na Mhe. Job Y. Ndugai, Mb, Spika. Wajumbe hao ni pamoja na;

- i. Mhe. Selemani J. Zedi, Mb
- ii. Mhe. Ali Ali Saleh, Mb
- iii. Mhe. Jamal K. Ali, Mb
- iv. Mhe. Esther M. Mmasy, Mb
- v. Mhe. Cecilia Paresso, Mb

Wajumbe hao walihudhuria na kushiriki kikamilifu katika Vikao vyote pamoja na mijadala. Mathalani, Mhe. Ali Ali Saleh mbali ya kuchangia Hoja ya mbalimbali aliwasilisha Hoja iliyoandaliwa na Bunge la Tanzania kwa niaba ya Ujumbe wa Tanzania. Hoja hiyo ilikubaliwa na Wajumbe na Mapendekezo yake kuwa mionganini mwa Maazimio ya Mkutano huo.

Mhe. Esther Mmasy mbali ya ku- *Second Motion* ya Kamati ya *Food, Agriculture and Natural Resources* pia alichangia Hoja ya Taarifa ya Mhazini, Mhe. Cecilia Paresso mbali ya kwamba ndio ilikuwa mara ya kwanza kuhudhuria Mkutano wa SADC PF alichangia Hoja ya Kamati ya *Human and Social Development and Special Programs*, Mhe.

Seleman Zedi alishiriki Vikao vyote vya Kamati ndogo ya Fedha na Kamati ya Utendaji na kwenye Plenary ali Second Motion ya Mhazini na Mhe. Jamal K. Ali alichangia Hoja ya Mhazini na Kamati ya *Democracy, Governance and Human Rights.*

Mambo yaliyojadiliwa katika Mkutano Mkuu wa 42 yakihuisha Tanzania ni kama ifuatavyo;

i) Deni la mchango wa Uanachama

Taarifa ya Kamati ndogo ya Fedha pamoja na Taarifa ya Mhazini ilionesha kuwa Tanzania inadaiwa Randi 2, 552,852/= ikiwa ni mchango wa mwaka wa fedha 2017/2018 ikiwa ni wajibu wa kila Mwanachama wa SADC PF kulipa mchango/ada ya uanachama.

Hata hivyo, wakati Mhe. Spika anachangia Hoja ya Kamati ya pamoja ya ya *Gender Equality, Woman's Advancement and Youth Development, Trade, Industries, Finance and Infrastructure and Regional Woman's Parliamentary Caucus* kwenye Mkutano Mkuu aliahidi kuwa Tanzania italipa deni hilo ndani ya muda mfupi.

ii) Mradi wa SRHR (Afya ya Uzazi Salama na Masuala ya UKIMWI)

Kamati ya *Human and Social Development and Special Programmes* ambayo inasimamia Mradi huu ilitoa taarifa kuwa Tanzania inasuasua katika kutekeleza mradi tajwa hapo juu pasipo kueleza sababu hasa wakati mradi huo unaufadhili wa asilimia 100.

Baadhi ya Wajumbe wakati wa uchangiaji walipendekeza nchi zinazosuasua kutekeleza mradi huo zinyanganywe na kupewa nchi zinazohitaji.

Hata hivyo, Tanzania bado wamepewa nafasi yakuendelea kutekeleza Mradi huo ingawa umebaki miezi mitatu kufikia ukomo.

iii) Mpango wa kumuendeleza Mtoto Wa Kike

Mwenyekiti wa Wajumbe Wanawake (*Regional Woman's Parliamentary Caucus*) wa SADC PF Dkt. Jassie Kabwili kutoka Malawi alilaumu msimamo wa Serikali ya Tanzania wa kutoruhusu Mwanafunzi wa Kike aliyepata ujauzito kurejea Shuleni baada ya kujifungua. Alieleza kuwa msimamo huo unamnyima Mtoto wa Kike Haki ya Msingi ya kupata elimu.

Aidha, Mwenyekiti huyo pia alilaumu kitendo cha Tanzania kuwakamata raia wa Afrika Kusini ambao waliingia Tanzania kwa madai kwamba wanafanya utafiti juu ya Haki ya mahusiano ya kijinsia nchini.

6. CHANGAMOTO

- Kutokuwa na mtiririko mzuri wa ushiriki wetu kunatokana na changamoto iliyopo sasa ya upatikanaji wa fedha za safari kwa wakati.
- Uchelewaji wa taarifa hasa za vikao Kamati. Ushiriki wa Wajumbe katika vikao vya Kamati umekuwa na changamoto nyingi kwa barua za mialiko kuchelewa kufikia Mabunge husika. Hii inatokana na shghuuli hizo za Kamati kutegemea zaidi ufadhili kutoka Taasisi mbalimbali.

7. HITIMISHO

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wawakilishi wenzangu naomba kutoa shukrani kwa utaratibu huu wa kuwasilisha taarifa kwa Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (2) (3), Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Huu ni utaratibu mzuri unaowezesha Bunge letu kupitia Kamati hii kufahamu mambo mbalimbali yanayoamuliwa kikanda na kusimamia utekelezaji wake wa

ndani ya nchi (*Domestication*). Mapendekezo yetu kuwe na utaratibu wa kuwakutanisha Wabunge wote kwa pamoja ili vyama hivi vy a Kibunge viweze kueleza shughuli mbalimbali zinazofanywa na vyama ili kuwa na ufahamu wa pamoja.

Aidha, kwa ushauri tunaomba taarifa za vyama hivi vy a Kibunge ziwe zinawasilishwa katika kipindi cha Kamati kuelekea Bunge la Bajeti Machi/Aprili kwani kwa kipindi hicho vyama vingi vinakuwa vimeshatekeleza majukumu yake mengi tangu kuanza kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wawakilishi wa Bunge la Tanzania kwenye SADC PF naomba kuwasilisha.

Selemani J. Zedi, Mb

22 Januari, 2018

Kwa niaba ya Wajumbe wawakilishi